epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Alhamisi Desemba 19, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581895
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
Nipashe digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710
LIKE & FOLLOW US

# Makada wakusanyika maskani kwa Mbowe

• **Wamo** wenyeviti CHADEMA mikoa 20, viongozi wa dini wakimwomba agombee tena, mwenyewe ajipa saa 48; Lissu arejesha fomu... *Ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akisalimiana na wafuasi wake waliokwenda nyumbani kwake Mikocheni, Dar es Salaam jana ili kumwomba agombee tena nafasi ya uenyekiti wa chama hicho. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

UKURASA WA 2

**TEC**, wanasheria wafanya tathmini Uchaguzi S/Mitaa



UKURASA WA 8

**Bodaboda** anusurika, wenzake waenda jela maisha kesi ya 'unga'



UKURASA WA 5

**Polisi**, mshukiwa wafa wakirushiana risasi katika msako

## Ajali ilivyokatisha uhai wa watu 15, kujeruhi saba

UKURASA 18

## Vijana wataka umri kustaafu uwe miaka 50

UKURASA 5

**MICHEZO** YANGA, MASHUJAA MECHI YA KIUFUNDI UK.24 **MAONI,** UK.6

# Makada wafurika nyumbani kwa Mbowe

**Elizabeth Zaya na Enock Charles**



MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema atatoa msimamo wake ndani ya saa 48 zijazo kama atagombea tena nafasi hiyo au la.

Alitoa kauli hiyo jana baada ya kuombwa na makada, wanaojumuisha wenyeviti wa chama hicho katika mikoa mbalimbali nchini pamoja na wafuasi wengine waliofurika nyumbani kwake Mikocheni, Dar es Salaam.

"Nimesikia na ninaheshimu maombi yenu. Nimepokea maombi na ushauri kutoka kwa makundi mbalimbali ya wanachama na wasio wanachama wakiwamo viongozi wa dini.

"Ninawaomba mnipe muda, nitaangalia ndani ya saa 48 nitatoa msimamo wangu mbele ya wahariri wa vyombo vya habari. Kama nitaona mambo hayaendi vizuri, mwamba nitaingia tena mzigoni," alisema Mbowe.

Kuhusu msuguano wa makundi ndani ya chama hicho kuelekea uchaguzi, Mbowe alisema hafurahishwi na hali hiyo na anawataka wanachama kuacha mivutano hiyo bali wawe kitu kimoja na waangalie mbele katika kujenga taasisi hiyo.

"Sijapenda makundi namna yanavyoendelea kusigana, kununiana, kuchukiana na pengine kusema uongo. Chama hiki kinaongozwa na vikao na si matamko ya Mwenyekiti Mbowe, mimi ni kiongozi tu.

"Anapotoka kiongozi aliyekaa miaka 20 madarakani na kusema jambo la tofauti, tunaanza kufikiri labda mwenzetu hatukuwa pamoja, kila mtu anayetafuta uongozi atafute lakini katika mazingira ya kuwajenga wenzake na kuilinda hii taasisi," alitoa angalizo.

Mbowe alisema amekuwa na wakati mgumu na familia yake inamshawishi kuachana na siasa, huku wanachama wa CHADEMA wakimshawishi kuendelea kuongoza chama hicho.

**UCHAGUZI**

Akizungumzia uchaguzi ndani ya chama hicho, Mbowe alionya makundi kusigana na kuchafuana kwa kutumia uongo, huku akitamba historia ya uongozi wake ndani ya chama inambeba.

Hivyo, aliwataka wanachama wa chama hicho kulinda chama hicho kwa wivu mkubwa, kutokuwa na kinyongo na mtu yeyote pasipo kufanya ulipizaji kisasi na kwamba hata yeye amewasamehe wote waliokuwa wamemtukana na kumdhalilisha kwa maneno mbalimbali katika mitandao ya kijamii.

Mbowe alisema: "Kuna maisha baada ya uchaguzi, hivyo tusiwadhalilishe wenzetu kwa kuwa ni askari wenzetu na wapiganaji wenzetu. Mimi nimewasamehe wale wote waliokuwa wananitukana na wanaoendelea kunitukana."

**ILIVYOKUWA NYUMBANI**

Nje ya nyumba ya Mbowe, baadhi ya wafuasi wa chama hicho pamoja na wenyeviti kutoka katika zaidi ya mikoa ya kichama 20, ni miongoni mwa waliojitokeza kumwomba na kumshawishi mwanasiasa achukue fomu ya kutetea tena nafasi yake.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi hao, Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Iringa, William Mungai alisema watamuunga mkono Mbowe katika uchaguzi wa kitaifa wa chama hicho unaotarajiwa kufanyika Januari mwakani ikiwa atagombea.

Viongozi hao pamoja na mamia ya wafuasi walifika nyumbani kwa Mbowe saa nne asubuhi, baadhi wakitumia magari binafsi, mabasi madogo ya abiria (coaster) na bodaboda. Walifurika nyumbani kwake.

Saa 9:25 alasiri Mbowe alitoka ndani ya nyumba yake kuwasikiliza wafuasi hao pamoja na wenyeviti. Hapo ndipo Mwenyekiti wa Mkoa wa Iringa, Mungai, aliposema kuwa kutokana na ubunifu wa Mbowe, CHADEMA imeendelea kuwa imara kwa miaka mingi.

Mungai alitaja sababu zilizowasukuma kumwomba mkongwe huyo wa siasa agombee tena nafasi yake, ni ububifu wa opereshieni mbalimbali ambazo zimewezesha chama hicho kupata wanachama, zikiwamo Operesheni Sangara na Movement for Change na kwamba hawana uhakika na wagombea wengine iwapo watasaidia katika kuongeza wanachama.

Alisema amebuni nguo, bendera na alama nyingine za chama ambazo zimepata umaarufu na zinatumika mpaka leo.

Mungai alisema Mbowe ana uwezo wa kujenga viongozi ambao wengine wamechukuliwa na vyama vingine na kuwa viongozi katika vyama hivyo, wengine kupata uongozi serikalini; wakijumuisha wakuu wa wilaya, mikoa na hata mawaziri.

Alisema Mbowe ni 'States Man' na jasiri wa vita asiyeogopa mapambano na siyo mtu wa matamko tu kama wengine, akitolea mfano alivyoweza kujitokeza katika maandamano waliyoyatangaza miezi iliyopita, tena akiwa na binti yake.

Makamu Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani, Ally Kadogoo alisifu uongozi wa Mbowe kuwa ni wa kutoa fursa sawa kwa watu wote, akijitolea mfano, kwamba alipotoka, hakuwahi kuwa hata mjumbe wa mtaa lakini hivi sasa ni Makamu Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani.

**LISSU ARUDISHA FOMU**

Wakati wafuasi wakijitokeza nyumbani kwa Mbowe, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu jana alirudisha fomu ya kuwania nafasi ya uenyekiti wa chama hicho.

Lissu alifika katika makao makuu ya chama hicho majira ya mchana na kupokewa na Naibu Katibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Benson Kigaila.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# TEC, wanasheria wafanya tathmini ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI mbalimbali wa dini na wadau wa siasa wametoa tathmini kuhusu kilichojiri katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji uliofanyika Novemba 27 mwaka huu.

Wamesema licha ya malalamiko ya raia na watu wenye nia njema, serikali haikuchukua hatua zozote za kurekebisha.

Rais wa Baraza la Maaskofu Kanisa Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Wolfgang Pisa, aliyasema hayo jana katika mkutano uliokutanisha viongozi hao wa dini kutoka madhehebu mbalimbali ya kikristo nchini katika ukumbi wa TEC Kurasini, Dar es Salaam.

Maaskofu hao pamoja na wadau wengine wa masuala ya amani na haki, wamekutana kufanya tathmini ya uchaguzi huo uliofanyika Novembа 27, mwaka huu, chini ya mada isemayo, 'Je, Uamuzi wa Wapigakura Umeheshimiwa?'.

Akisoma tathmini hiyo, Pisa alisema: "Maeneo mengine tukiri uchaguzi ulifanyika kama mchezo mchafu uliosababisha vifo vitisho, rushwa, ufisadi, upendeleo, wizi wa kejeri kwa wapigakura na wagombea.

Licha ya malalamiko ya raia na watu wenye nia njema, serikali haikuchukua hatua zozote. Hii ni tabia mbaya sana inayobomoa taifa, maadili ya kisiasa, kiuchumi na kuharibu mfumo wa uwajibikaji kwa viongozi wa raia."

Askofu Pisa alisema kupata viongozi kwa mtindo huo ni wananchi kupewa viongozi ambao hawakuwachagua.

"Imefika mahali kila inapotokea uchaguzi thamani ya utu, uhai na maisha ya Mtanzania vinashushwa kwa utekaji, mauaji na aina yote ya ukatili," alisema.

Askofu Pisa alisema wakifungamana na ukweli na kuusimamia, utawafanya wawe huru dhidi ya mambo mbalimbali na nchi yao.

"Tufanye tafakari mbalimbali tukijua tunawajibika mbele ya Mungu, mbele ya watu na mbele ya taifa letu, Mungu ambaye hadanganyi wala hadanganyiki atuongoze," aliwaeleza washiriki wa mkutano huo.

Askofu Pisa alisema uchaguzi wowote unaofuata mwongozo wa kikatiba na kisheria ni tendo linalohusisha uhuru, haki na dhamiri ya raia husika. Alisema ili kuhakikisha haki ya raia inaheshimika, mchakato wote wa uchaguzi husimamiwa ili ufanyike kikatiba.

"Ibara ya 3,5, 21 ili kuhakikisha hili yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa, moja, wenye sifa za kupiga kura wameandikishwa, pili, wagombea wenye sifa ya kuomba na kuteuliwa kwa mujibu wa vyama husika.

"Tatu, kampeni za wagombea na ushindaji wa vyama hufanyika kwa haki na katika fursa sawa bila upendeleo wowote, nne, wapiga kura husikiliza kampeni ili kufanya uamuzi wa msingi wa hoja na uwezo wa wagombea katika kuongoza," alisema.

"Tano, wapiga kura huwekwa katika mazingira ya faragha ili kuheshimu usiri wa kura yao wakiamini baada ya kupiga kura inahesabiwa kwa haki na katika uangalizi wa haki uliokubalika," aliongeza.

Alitaja jambo la sita ni wasimamizi na waratibu kuheshimu uamuzi wa kila mpigakura na saba, vyama kuwa na mawakala wao, kushuhudia upigaji kura kwa heshima, faragha na usiri bila bughudha au vishawishi vya aina yoyote.

"Nane, matokeo ya kweli ya uchaguzi huthibitishwa na vyama husika na kutangazwa bila kuingiliwa na chombo kingine na tisa, kuwa na fursa ya kuhoji na kupinga matokeo kama kuna shida au dosari".

Askofu Pisa alisema wameshuhudia katika uchaguzi huo, hivyo ni juu yao kujiuliza yaliyotajwa ndiyo yaliyofanyika.

"Tuliyasikia matokeo ya uchaguzi yaliyotolewa na mamlaka husika kwa mujibu wa sheria zetu. kila mmoja anaweza kujibu swali hili, Je, uchaguzi na matokeo yake uliendeshwa kwa uwazi, haki na uhuru?

"Viongozi wa dini tuliokabidhiwa kondoo wa Bwana kuwachunga na kuwalisha, tukiongozwa na ukweli na kulinda utu wa mwanadamu, katika kikao hiki tupate nafasi ya kutathmini vizuri yaliyopita.

"Waheshimiwa viongozi wa dini na wengine mlioalikwa, kama alivyoeleza Katibu Mkuu wa TEC, sisi ni walezi wa kiroho na walinzi wa kimaadili. Dhamira ya jamii ni juu yetu kulinda umoja katika taifa letu," alisema.

Alisisitiza kwamba, wao ni sauti ya kinabii inayotetea haki za kibinadamu pia ni sauti ya wale wasioweza kusema, wanaonyimwa haki zao za msingi kama ile ya kupata viongozi kwa njia ya haki, hivyo aliwataka kutathmini hali ya uchaguzi ulivyokwenda, maandalizi na mipango ya awali yalihusisha kwa kiasi gani wapigakura na vyama husika.

"Maofisa husika walikuwa na maadili kiasi gani katika suala la usimamizi? Uandikishaji wapigakura ulikwendaje? wananchi walikuwa na elimu ya kutosha? Mchakato wa uteuzi wagombea ulikwendaje? Mazingira ya kufanya kampeni yalikuwa sawa kwa wagombea wote na mazingira na vituo vya kupigia kura yalikuwa huru?" alisema.

Pia aliwataka kutathmini kama hatua ya kuhesabu na kutangaza matokeo zilifanyika bila kuleta maswali yoyote.

"Lengo hapa si kutafuta makosa. Sehemu ambayo uchaguzi ulikwenda vizuri tupongeze na tuchukue kama kiwango cha kufanya vizuri zaidi siku zijazo," alisisitiza.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

# Mwinyi asisitiza utawala bora kwa maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema suala la kuimarisha utawala bora ni jambo la msingi ili kuleta maendeleo ya nchi.

Kutokana na umuhimu huo, amewasihi watumishi wa umma na sekta binafsi binafsi kuongeza juhudi, uzalendo na uadilifu katika kulitumikia taifa.

Dk. Mwinyi, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na idara ya mawasiliano Ikulu, Zanzibar, aliyasema hayo jana katika ukumbi wa Ziwani Polisi Zanzibar kwenye maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Ukaguzi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Zanzibar.

Alisema wajibu wa kuimarisha utawala bora hasa kwa matumizi ya rasilimali za umma, si wa serikali na ofisi ya CAG pekee bali ni kwa kila mtumishi.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, alisema itaendeleza juhudi za kuijengea mazingira mazuri ofisi ya CAG ili itekeleze vizuri kazi zake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo kitaifa na kimataifa na kwenda sambamba na mabadiliko ya mara kwa mara ya ukaguzi duniani.

Dk. Mwinyi alibainisha kuwa ofisi ya CAG imeisaidia serikali kutekeleza kwa ufanisi malengo na mipango yake. Alisema maendeleo makubwa yaliyofikiwa serikalini yanatokana na mchango wa udhibiti na ukaguzi bora wenye kuzingatia uwajibikaji, nidhamu na uwazi katika matumizi ya rasilimali za umma.

Rais Mwinyi pia alisema miongoni mwa faida zinazopatikana kwenye ofisi ya CAG ni pamoja na kusaidia kuongeza pato la serikali na CAG kupitia ripoti yake ya kila mwaka, huishauri serikali juu ya mbinu bora za kuziba mianya ya upotevu wa makusanyo ya mapato ya serikali, kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuwapo kwa usimamizi bora wa rasilimali za umma.

Alisema ufanisi unaotokana na utekelezaji wa kazi za ukaguzi una mchango mkubwa kwa serikali hasa kuimarisha uchumi wa Zanzibar na hadi kufikia mwaka 2023 kasi ya ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa 7.4% ikilinganishwa na 1.3% ya mwaka 2020.

Dk. Mwinyi aliongeza kuwa mafanikio ya kazi za ukaguzi wa rasilimali za umma, yameimarisha utoaji wa huduma za jamii ikiwamo elimu, afya, majisafi na salama, nishati ya umeme na huduma zingine.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, Dk. Othman Abbas Ali, alibainisha kuwa maadhimisho hayo ni fursa adhimu kwa taasisi za umma kuwatumia wataalamu wao kuongeza uwajibikaji, kubadilishana uzoefu na kujifunza mbinu bora za kukabiliana na uhujumu wa uchumi, kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Aliongeza kuwa kujadiliwa kwa ripoti za CAG kila mwaka katika Baraza la Wawakilishi kumeendelea kuleta tija ya usimamizi wa rasilimali na matumizi ya fedha za umma kwa taasisi mbalimbali na kujenga uelewa kwa wananchi juu ya utendaji wa ofisi hiyo.

Maadhimisho ya Wiki ya Ukaguzi ya ofisi ya CAG Zanzibar kwa mwaka 2024, yenye kauli mbiu isemayo "Kuimarika kwa Ukaguzi wa Rasilimali za Umma Kunaongeza Ufanisi na Kuleta Tija Nchini" yalianza Desemba 12, mwaka huu na kufikia kilele jana.



Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Leonard Bandola, akitoa elimu kwa abiria katika mabasi yanayosafiri kwenda mikoani, kuelekea sikukuu ya Krismasi na Mwaka mpya, kuwa na tahadhari ya kuepuka matapeli na kutoa taarifa kwa madereva wanaovunja sheria za usalama barabarani wakiwa njiani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Dk. Manguruwe aandika barua kwa DPP kukiri kosa

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI mwanzilishi wa Vanilla International Limited, Simon Mkondya, maarufu Dk. Manguruwe, anayeshtakiwa kwa kesi ya uhujumu uchumi, amemwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ya kuingia makubaliano ya kukiri kosa (plea bargaining).

Dk. Manguruwe pamoja na Rweyemamu John ambaye ni mkaguzi wa kampuni hiyo, wanashtakiwa kwa mashtaka 28 yakiwamo ya kujipatia zaidi ya Sh. milioni 90 kwa udanganyifu na utakatishaji, kwa kununua viwanja tisa eneo la Idunda mkoani Njombe.

Wakili wa Serikali, Winiwa Kashala, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Anna Magutu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa kesi hiyo imeitwa kwa ajili ya kutajwa na pia upelelezi bado haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hata hivyo, alidai kuwa Dk. Manguruwe ameandika barua ya 'plea bargaining' lakini hawajakubaliana na ombi hilo hadi upelelezi wa kesi hiyo ukamilike.

Hakimu Magutu aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 2, 2025 kwa kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi itakapofikia. Dk. Manguruwe anaendelea kusota rumande kwa sababu anashtakiwa kutakatisha Sh. milioni 90.

Mshtakiwa wa pili aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya kuwa na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho na kuwasilisha hati ya mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 45.

Ilidaiwa kwamba washtakiwa hao walitenda makosa hayo katika tarehe tofauti kati ya Januari Mosi, 2020 na Desemba Mosi, 2023 ndani ya mkoa wa Dar es Salaam.

Ilidaiwa kwamba mashtaka 19 ni ya kufanya biashara ya upatu. Katika kipindi hicho Mkondya akiwa mkurugenzi na John akiwa mfanyakazi wa kampuni hiyo, wanadaiwa kufanya biashara ya upatu kwa kuwaahidi watu kupata faida mara mbili hadi tatu kulingana na kiasi cha fedha watakazotoa.

Ilidaiwa kwamba washtakiwa hao walijipatia kiasi cha jumla ya Sh. milioni 92.2 kutoka kwa watu 19 tofauti na watu hao walitoa kiasi tofauti cha fedha na aliwaahidi watapata faida mara mbili hadi tatu ya fedha walizotoa.

Iliendelea kudaiwa kwamba, mashtaka tisa ni ya utakatishaji yanayomkabili Mkondya pekee na kwamba kati ya Januari Mosi, 2020 na Desemba Mosi, 2023 akiwa kama mkurugenzi wa kampuni hiyo, alijipatia viwanja tisa kitalu namba AB eneo la Idunda mkoani Njombe huku akijua viwanja hivyo ni mazalia ya makosa tangulizi ya upatu.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## Vituo 47 vya kufundisha Kiswahili vyaanzishwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi amesema serikali kupitia Baraza la Kiswahili Tanzania, imeanzisha vituo 47 vya kufundisha lugha ya Kiswahili ili kukuza na kueneza lugha hiyo duniani.

Alisema hayo wakati akifungua kongamano la siku mbili la kimataifa la utamaduni lijulikanalo kama Afrika ya Kesho linalofanyika katika Chuo Kikuu cha Jordan (JUCO) mjini Morogoro. Kati ya vituo hivyo, 17 viko nje ya Tanzania.

Alisema taasisi za elimu ya juu kupitia vijana zinaendelea kufanya utafiti na kuibua mijadala ya kutafuta urithi wa utamaduni unaoshikika na usioshikika ili kusaidia kurudisha utamaduni wa kiafrika kwa maslahi mapana ya bara la Afrika.

Msemaji Mkuu wa kongamano hilo linaloandaliwa na vyuo vikuu na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya Tanzania, Prof. Anna Tibaijuka alisema kuwa na lugha moja ya asili kunabeba vitu vingi vya kiutamaduni, hivyo Afrika haipaswi kupoteza Kiswahili na kwa kufuata lugha za kigeni.

"Hatuwezi kuondoa lugha hii kwa namna yoyote ile, lazima tulinde Kiswahili, lakini na lugha zetu za makabila yote, na kwenye hili lazima tusiweke ukabila," alisema Prof. Tibaijuka.

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Jordan, Bertram Mapunda alisema kizazi cha sasa kinaamini kuwa mambo ya utamaduni na kuzungumza lugha za asili ni wazee wa zamani na siyo wa sasa, hivyo akawataka vijana kujifunza lugha za asili ili kusaidia kukuza na kueneza lugha hiyo.

Kuhusu elimu ya juu, Mapunda alisema wanakusudia kuanzisha mitaala watayoweza kuingiza namna ya kufundisha lugha za asili kwa wanafunzi ili kuendelea kukuza na kueneza lugha hizo.

Kiongozi wa kimila kutoka kabila la Maasai, Chifu Mtayani Simanga alisema kupitia kongomano hilo viongozi wa asili walikusudia kuonana na viongozi wa nchi ili kuwaeleza namna sahihi ya watu kuishi majumbani ili kurejesha hali ya amani na utulivu katika bara la Afrika.

Kongamano hilo limeandaliwa na Chuo Kikuu cha Jordan JUCO kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Waislamu (MUM), Chuo Kikuu cha Zanzibari, Chuo Kikuu cha Zimbabwe, Chuo Kikuu cha Nigeria na Taasisi ya Arizona ya Marekani (PPEP).

# Ndumbaro aahidi kumaliza migogoro wakulima, wafugaji

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema anatarajia kuanzisha oparesheni maalum ya kukomesha migogoro ya wafugaji na wakulima katika Wilaya na Kilosa na mkoa wote wa Morogoro.

Dk. Ndumbaro alisema hayo juzi wilayani Kilosa ikiwa ni mwendelezo wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayofanyika kwa siku 10 katika mikoa ya Morogoro, Songwe, Mara na Iringa.

Alisema hawako tayari kuona mkoa huo unaendelea kuwa kinara wa migogoro hiyo kwa wafugaji na wakulima na kwamba wamejipanga kuja na mbinu mbadala ya kukomesha hilo.

"Kilosa ndiyo makao makuu ya migogoro ya wakulima na wafugaji kwenye nchi hii. Yaani nchi nzima migogoro hii iko hapa zaidi. Hatutakubali hali hii iendelee, hivyo tumedhamiria kuibomoa hii ikulu ya migogoro hapa," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema kwa kuanza kuibomoa migogoro hiyo, wanaanza kutumia siku hizo 10 za Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia na baada ya hapo wataandika ripoti kama kuna mahali kutakuwa kumebaki na tatizo waje na oparesheni nyingine ili waimalizie kabisa.

"Na tunaanza oparesheni yetu ya kuibomoa migogoro hii kwa kutumia siku hizi 10 za kampeni ya msaada wa kisheria inayoendelea, na baada ya kumalizika kwa kampeni hii kama kutakuwa kuna mahali kumebaki, tutakuja na oparesheni nyingine ya pili ya kumalizia kabisa mpaka iishe, hatutaki ibaki tena,"alisema Dk.Ndumbaro.

Alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilosa, kufanya tathmini baada ya kampeni hiyo ya siku 10 ili kufahamu kazi iliyofanyika na kufahamu mahali ambapo kumebaki na tatizo ili wajipange tena namna ya kulitatua.

"Natamani migogoro iondoke kabisa. Na mimi niseme kabisa kwamba baada ya siku hizi 10 itaandikwa ripoti yenye kuainisha migogoro ipi imekwisha na ipi imesalia, lengo ni kuhakikisha tunaimaliza.

"Ile ambayo imesalia, tutakuja na oparesheni maalumu nyingine ambayo tutakuwa tunaweka tenti , kusikiliza na kuimaliza papo kwa papo na hiyo itakuwa kama mahakama," alisema.

Dk. Ndumbaro aliwataka wananchi kutumia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia kwenda kufuatilia haki zao.

Mkuu wa mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema migogoro mingine iliyoko katika mkoa huo ni ile inayohusu jamii hususani katika eneo la ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.



Ofisa wa Wizara ya Afya, Peter Gitanya, akieleza namna utekelezaji wa mpango wa ugawaji vyandarua ngazi ya kaya wakati wa kikao cha maandalizi ya ugawaji wa vyandarua hivyo, ifikapo Januari 16 mwakani, kilichofanyika Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# KOICA yaahidi kuboresha huduma za afya nchini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Kimataifa la Misaada la Jamhuri ya Korea (KOICA) limeahidi kuendelea kusaidia Serikali ya Tanzania kuimarisha huduma za afya na kuboresha miundombinu ili kuleta maendeleo kwa wananchi.

Ahadi hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkazi wa KOICA nchini, Manshik Shin wakati hafla ya kukabidhi Kituo cha Afya Ilazo jijini kwa ajili ya kutoa huduma ya uzazi, mama na mtoto kilichojengwa kwa thamani ya zaidi ya Sh. bilioni saba.

Shin alisema shirika hilo litaendelea kusaidia serikali ili kuhakikisha inatoa huduma bora kwa jamii katika maeneo mbalimbali nchini.

KOICA kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) wamejenga kituo hicho ambacho ni kati ya vinne vyenye thamani ya Sh. bilioni 20 chini ya mradi wa mama na mtoto uliotekelezwa kwa miaka mitano mkoani Dodoma.

Akizungumza jana wakati wa makabidhiano hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alisema kituo hicho kitatoa huduma kwa wakazi wa kata za Ipagala na Nzuguni.

Alisema ujenzi huo unatokana na uhusiano mzuri kati ya Serikali ya Korea na Tanzania.

Alisema kituo hicho kina jengo la huduma za upasuaji wa dharura na kituo cha damu salama.

Balozi wa Jamhuri ya Korea nchini, Eunju Ahn, alipongeza mageuzi yanayofanywa na serikali kwenye Sekta ya Afya kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita na kuahidi kuendelea kushirikiana ili kuboresha zaidi sekta hiyo.

Mwakilishi Mkazi wa UNICEF, Elke Wisch alisema kupitia uhusiano huo, huduma za afya jumuishi zimewafikia watu walio katika mazingira magumu nchini.

Wisch alisema Tanzania itaboresha huduma za dharura za upasuaji na kuhimiza mradi huo kutunzwa ili kuhudumia jamii kwa muda mrefu.

Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# RC ajivunia ujenzi vituo vya polisi

**Na Fredy Mgunda,** LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack amezindua kituo cha polisi wilaya ya Lindi, akikitaja kitaongeza ufanisi wa kazi wa jeshi hilo katika kulinda amani na majukumu mengine.

Akizundua kituo hicho, Zainab alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassani kulitazama jeshi hilo hasa kwenye kuboresha miundombinu ya kufanyia kazi na usafirishaji wa watendaji wake.

Telack pia alitumia fursa hiyo kupongeza jeshi hilo kwa kazi kubwa ya kusimamia amani na kufanya mkoa wa Lindi kuwa wenye utulivu wakati wote.

Katika hotuba yake ya kumkaribisha mgeni rasmi huyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi John Imori alisema ujenzi wa kituo hicho daraja "A" ulianza mwaka 2022 na kukamilika 2023, mkandarasi wa mradi huo akiwa ni fundi mkuu wa Kikosi cha Polisi cha Ujenzi.

Mradi huo umegharimu Sh. milioni 948.334.

Sambamba na ujenzi huo, Kamishna Msaidizi Omori alitaja miradi mingine ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya polisi vinayoendelea katika hatua mbalimbali ndani ya mkoa wa Lindi.

Hiyo ni pamoja na ujenzi wa kituo cha polisi daraja "C" na nyumba mbili za makazi ya askari katika kata ya Nandagala, wilayani Ruangwa unaogharimu Sh. milioni 164 na ujenzi wa kituo cha polisi daraja "C" kwenye kata Kibutuka, wilaya ya Liwale Sh. milioni 115.

Miradi mingine ni ujenzi wa kituo cha polisi daraja "C" kata ya Somanga, wilayani Kilwa Sh. milioni 115, ujenzi wa kituo cha polisi daraja "C" kata Tingi wilayani ya Kilwa Sh. milioni115, ukarabati wa kituo cha polisi kata ya Naipanga, wilaya ya Nachingwea Sh. milioni 52 na ukarabati wa Kituo cha Polisi Nanjilinji, kata ya Nanjilinji wilayani Kilwa Sh. milioni 15.

Mkuu wa Mkoa Zainab pia alitumia jukwaa hilo kuwaomba viongozi wa dini kuwaombea watoto ambao wako katika hatari ya matendo ya ukatili wa kijinsia na mmomonyoko wa maadili.

## HABARI KITAIFA

## Askari polisi wawili wafariki dunia katika majibizano ya risasi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WATU watatu wakiwamo askari polisi wawili, wamefariki dunia katika kijiji cha Msagali, wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma katika mapambano ya kurushiana risasi wakati wakimkamata mtuhumiwa wa unyang'anyi wa kutumia silaha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, alisema jana saa saba usiku baada ya mtuhumiwa Atanasio Malenda (30) kudaiwa kumpora Yohana Lameck Sh. milioni mbili kwa kutumia silaha.

Aliwataja askari waliofariki dunia kwenye tukio hilo kuwa ni Jairo Kalanda na Alfred John wakati mtuhumiwa Atanasio alifariki dunia alipokuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa.

Alifafanua kuwa askari hao wakiwa na wenzao, walipata taarifa kuwa mtuhumiwa huyo aliyekuwa anatafutwa yuko nyumbani kwake, Msagali.

"Walifika kijijini hapo na kutafuta uongozi wa kijiji na Kwenda nao nyumbani kwa mtuhumiwa huyo ambaye baada ya kufika, alitoka ndani na kuanza kuwashambulia askari. Katika majibizano hayo, ndipo vikatokea vifo hivyo,"alisema.

Pia alisema katika majibizano hayo askari Msuka na raia mmoja anayefahamika kwa jina la Msima Nyau, walijeruhiwa na wanaendelea na matibabu katika hospitali hiyo.

"Nitoe wito kwa wananchi watii sheria bila shuruti pindi wanapokamatwa na polisi hatua zaidi za kisheria zichukuliwe. Taratibu zinaendelea ndugu kuchukua miili ya marehemu kwa ajili ya mazishi,"alisema.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Vijana wataka umri wa kustaafu uwe miaka 50

**Na Maulid Mmbaga**

BAADHI ya vijana waliotoa maoni kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, wameshauri serikali kushusha umri wa kustaafu hadi miaka 50 kwa hiari na 55 kwa lazima kutoka 60 inayotumika sasa, ili kutoa fursa kwa vijana wengi zaidi kuingia katika mfumo wa ajira.

Akitoa maoni yake jana mkoani Dar es Salaam, Omary Punzi ambaye ni Mratibu wa Makongamano ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 Toleo la Mwaka 2024, alisema serikali inapaswa kuliangalia hilo kwa ukaribu ili vijana nao wale keki ya taifa.

Alisema ni vyema sekta binafsi nayo itengeneze mfumo wa maombi ya ajira kama ilivyo kwa mfumo wa Ajira Portal wa serikali, ili kijana anapotaka kwenda kujiunga na sekta hiyo aone ushindani, akidai kuwa sekta za umma kukitokea fursa zinatangazwa, lakini binafsi hali ni tofauti. Chache hutangazwa.

"Kadhalika, tunaona sasa hivi umri wa kuingia jeshini ni miaka 25, lakini tuna mfumo ambao serikali ilianzisha wa elimu ya watu wazima, lakini mfumo wa kuingia jeshini haujawapa kipaumbele wale ambao wanamaliza katika umri wa watu wazima.

"Ni vyema umri wa kuingia jeshini ukasogezwa ukafika angalau kuanzia miaka 30 ili wale ambao wamemaliza elimu ya juu wakiwa ndani ya umri huo wapate muda wa kujiunga na kulitumikia taifa lao," alishauri Punzi, ambaye pia ni Mratibu wa Shughuli za Skauti Mkoa wa Pwani - Idara ya Kazi Maalumu.

Naye Saimon Chambi alishauri kwamba kuelekea mwaka 2050, kuwapo jukwaa na mkakati maalumu wa kuwaunganisha vijana na fursa mbalimbali za ajira na programu za kimataifa za kubadilishana uzoefu kama sehemu ya kuondoa kundi hilo katika changamoto ya ajira.

Alisema asilimia tano pekee ya vijana ndiyo wanaonufaika na fursa mbalimbali za mafunzo na ajira nje ya nchi na hivyo kutaka kuundwa kwa mkakati maalumu kuwawezesha kupata taarifa sahihi za fursa hizo na kutengenezwa njia nyepesi kwa kundi hilo kujiunganisha na ajira na mafunzo.

"Dira ya 2050 iainishe namna ambavyo vijana wanaweza kupata mafunzo mbalimbali ya mambo yasiyofundishwa kwenye taasisi rasmi za elimu, ikiwamo afya ya uzazi, elimu ya fedha na mengineyo ili kusaidia kundi hilo kujitambua na kutumia vyema rasilimali fedha kidogo wanazopata kwa njia mbalimbali," alishauri Chambi.

Gipson Kawago, akitoa maoni yake, alishauri kuwe na mkazo katika elimu ya vitendo zaidi kuliko nadharia, akisisitiza kuwa hiyo itawasaidia vijana baada ya kuhitimu kuwa rahisi kujiajiri.

"Kuna uhaba wa miundombinu rafiki ya kumwaandaa kijana kuwa na utaalamu wa kivitendo. Pia kuwe na utaratibu wa kuwafundisha wanafunzi kuhusu akili mnemba kuanzia shule za msingi ili isiwe jambo geni kwao wanapofika ngazi za juu, kwa sababu teknolojia inaendelea kukua," alisema Kawago.

Joseph Malekela alisema dira haijaonesha namna gani nchi imeweka mikakati ya kuwaandaa vijana katika kushiriki kwenye masuala mbalimbali ya uongozi, akishauri ni muhimu dira kuonesha utaratibu rasmi kufikia mwaka 2050 vijana watashiriki kwa kiasi gani katika nafasi za uamuzi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ridhiwani Kikwete, alisema atahakikisha kundi la vijana linaendelea kuwa sehemu ya wanufaika wa keki ya taifa kwa kufanyia kazi mawazo yao.

"Niwahakikishie kwamba mimi kama waziri wa vijana, nitayasimamia yale ambayo mmeyasema na nitahakikisha yote yaliyosema yanaakisi katika huo mpango mkubwa unaotakiwa kwenda kutokea. Moja ya vipaumbele vya Rais Samia Suluhu Hassan kuniteua ni ili kwenda kushughulikia changamoto za vijana," aliahidi.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Mkurugenzi wa Kampuni ya Vannila International Limited, Saimon Mnkondya maarufu kama Dk Manguruwe, akiwa chini ya Ulinzi wa Askari Magereza akielekea katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana kusikiliza kesi inayomkabili yenye mashtaka 29 ikiwamo ya uhujumu uchumi na kujipatia pesa kwa njia ya udanganyifu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kabudi: Tanzania itakuwa kinara uhuru wa habari

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema katika uongozi wake atahakikisha Tanzania inakuwa kinara wa uhuru wa vyombo vya habari duniani.

Aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na wadau mbalimbali wa habari kuhusu namna ya kushirikiana kukuza uhuru wa habari.

Prof. Kabudi alisema hata Rais Samia Suluhu Hassan aliwahi kusema vyombo vya habari si mshindani bali ni mdau muhimu wa serikali ambaye wanapaswa kushirikiana. Kwa mantiki hiyo, alisema hiyo ndiyo taa na dira kwake anapoanza kufanya kazi katika wizara hiyo.

Aidha, alisema kuongezeka kwa vyombo vya habari ni moja ya mafanikio makubwa ya kujivunia ya serikali.

Prof. Kabudi alisema ingawa serikali itaendelea kuenzi uhuru wa Habari, waandishi wa habari wanapaswa kuzingatia mipaka ya kikatiba iliyoko kwenye ibara ya 18 na ile ya 30 inayosema kila haki ina mipaka.

Alisema kwa mujibu wa ripoti ya vyombo vya habari ya mwaka 2024, Tanzania imeendelea kupanda kwa nafasi ya uhuru wa habari jambo ambalo Watanzania wanapaswa kujivunia.

"Nawaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana na vyombo vya habari ili tuendelee kuwa juu kwenye takwimu za kidunia kwa kuhakikisha vyombo vya habari vinaendelea kuwa huru lakini nanyinyi mzingatie miiko na maadili ya kazi zenu," alisema.

Waziri Kabudi alisema serikali imefanya mambo makubwa ya maendeleo kwenye maeneo mengi nchini, hivyo waandishi wa habari wana jukumu la kwenda kuchukua taarifa na kuzitoa.

"Kwenye hospitali mbalimbali za wilaya na zahanati kuna vifaa vya kisasa ambavyo zamani vilipatikana kwenye hospitali za mikoa na zile za rufani. Watumieni waandishi wa mikoani kuchukua taarifa hizo na kuhabarisha umma," alisema

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Gerson Msigwa, aliomba vyombo vya habari viendelee kushirikiana na serikali kuhabarisha umma kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo.

Alisema sekta ya habari ni muhimu katika kujenga taifa lenye uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa maendeleo kwa kupata taarifa muhimu.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alisema bado kuna changamoto ndogo ndogo za kufanyia kazi ili kuhakikisha vyombo vya habari vinakuwa huru.

"Serikali imeunda Bodi ya Ithibati, itaunda Baraza Huru la Habari lakini bado Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo ana uwezo wa kufungia chombo cha habari bila kupitia kwenye hizi bodi. Sasa hapo tunaona bado kuna changamoto ya kufanyia kazi,' alisema.

Balile alisema serikali inapoona waandishi wa habari wamefanya makosa wanapaswa kuwashitaki kwenye Baraza Huru la Habari au kwenye Bodi ya Ithibati badala ya yenyewe kuwa mlalamikaji, mshitaki na mtoa hukumu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wataalamu hawa wachukuliwe hatua kukiuka miiko na maadili

**MKAZI** wa Magugu, Babati mkoani Manyara, Juliana Obedy (44), amepoteza maisha baada ya wataalamu katika Kituo cha Afya Magugu kudaiwa kumcheleweshea huduma kituoni hapo kutokana na kugongwa na nyoka. Sababu hasa za kucheleweshwa kwa huduma hiyo ni madai kwamba wataalamu kutaka kulipwa Sh. 150,000 ikiwa ni gharama za matibabu.

Kwa mujibu wa mume wa mwanamama huyo, wataalamu hao wa afya kituoni hapo walimwambia anatakiwa kulipa fedha hizo ndipo apatiwe matibabu lakini hakuwa nazo kwa wakati huo.

Kutokana na hali hiyo, inadaiwa kwamba ili kuokoa maisha ya mke wake, Laizer aliomba kuweka rehani chombo chake cha usafiri, pikipiki lakini watu hao walimkatalia. Aliamua kufanya hivyo baada ya kuwaomba wamhudumie mwenza wake kwa ahadi kwamba fedha hizo zingefuata baadaye.

Laizer alidai kuwa wataalamu waliomkatalia ni wauguzi wawili na daktari mmoja na baada ya hatua hiyo walimpigia mganga mfawidhi ambaye naye alisisitiza kuwa ni lazima alipe kiasi hicho cha fedha ndipo mkewe ahudumiwe. Kutokana na hali hiyo, Laizer aliamua kwenda kutafuta fedha na kufanikiwa kupata Sh. 130,000 ndipo walipokubaliana aanze kupatiwa tiba.

"Daktari alipigiwa simu mara ya kwanza hakupokea, akapigiwa simu mara ya pili ndipo alipopokea akasema anakuja na alitoa huduma na mgonjwa kuandikiwa dawa," alisema Laizer.

Hata hivyo, alisema alipoenda duka la dawa aliambiwa anatakiwa kulipia Sh. 150,000 ambapo Laizer aliomba mgonjwa ahudumiwe na fedha itafuata, lakini wauguzi wawili na daktari mmoja waliokuwapo hawakukubali na kuamua kumpigia Mganga Mfawidhi simu na kujibiwa kuwa anatakiwa alipie Sh. 150,000 na kukata simu.

Laizer alisema baada ya kuvutana na wataalamu hao alitoka na kwenda kutafuta fedha aliporudi alitoa Sh. 130,000 na badala ya kuanza kutoa huduma, wataalamu hao walianza kupigiana simu ndipo mmoja alisikika akisema mgonjwa ahudumiwe. Hata hivyo muda mfupi baadaye, mkewe huyo alipoteza maisha huku akilalamika maumivu makali.

Tukio hilo si la kwanza kutokea kwa wagonjwa kupoteza maisha kwa kukosa huduma kwa sababu ya kukosa fedha. Takribani mwezi mmoja uliopita, Mariam Zahoro, aliyekuwa mjamzito, mkazi wa kijiji cha Mumbwi, Handeni mkoani Tanga, alifariki dunia katika Kituo cha Afya cha Kabuku kwa kukosa fedha. Mwanamke huyo alitakiwa kutoa fedha kwanza ndipo afanyiwe upasuaji wa uzazi.


Aidha, Desemba 28, 2023 katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, alifariki dunia yeye na mtoto tumboni baada ya kushindwa kufanyiwa upasuaji wakati wa uzazi kutokana na kukosa Sh. 150,000 alizotakiwa na daktari kulipa ndipo apatiwe huduma.

Hayo ni matukio machache yanayoripotiwa lakini yako mengi na yamesababisha vifo kwa wagonjwa, huzuni na majonzi kwa ndugu, jamaa na marafiki. Swali la kujiuliza ni je, wahudumu hao wa afya wamekosa utu na kusababisha binadamu wenzao kupoteza maisha kisa kukosa fedha? Kwa maneno mengine, wametanguliza fedha mbele badala ya kuwaonea huruma binadamu wenzao?

Vitendo hivi havipaswi kufumbiwa macho kwa sababu ni vya kikatili na vinagharimu maisha ya binadamu. Hakika ni vitendo vya kusikitisha na vinatia uchungu katika nyoyo za wanadamu wanaothamini ubinadamu na vinakweza utu wa mtu, hivyo wahusika wanatakiwa kuchukuliwa hatua kwa sababu hawana tofauti na wauaji wengine.

Mamlaka husika zinapaswa kuchukua hatua zikiwamo za kinidhamu na kusheria. Ni wazi kwamba madaktari hao na wauguzi wana leseni zinazotolewa na vyama vyao na mabaraza ya kitaaluma, hivyo ikithibitika wamefanya hivyo, wafutiwe pia leseni kwa sababu ya kushindwa kuheshimu maadili ya kazi na taaluma zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Kuendekeza dawa za kulevya, tena tukiiga, tutaishia pagumu

**MAISHA** na mienendo ya kisasa ni kawaida sana watu wakienda na wakati kwa sababu tu wanajifunza vitu mbalimbali kama vile mashine za namna tofauti.

Ni kweli matumizi ya mashine hizo ikiwamo kompyuta, tukiiga bila uangalifu, tutaishia pabaya kwenye jamii zetu.

Baadhi yetu hufanya visivyostahili, wakiamini ni mitindo ya kisasa, wengine wanakunywa pombe kupita kiasi, kutumia dawa za kulevya, pia wanaziuza, katika imani ni 'kwenda na wakati', baada ya kushuhudia ama kwenye runinga na simu, hata kompyuta.

Wanafanya hayo pasipo kuwaza madhara yake. Kundi kubwa la vijana limeshadhurika wakiishi hivyo, wameathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya, wakiishia kupoteza ama nguvu au uwezo wa kufanya kazi, vilevile hata uwezo wa kufikiri.

Dawa za kulevya ni kemikali. Zinapoingia mwilini huathiri ubongo wa mtumiaji, ukisababishia matendo, hisia, fikra na mwonekano tofauti.

Hizo ni kemikali zinazotokana na mimea na madini malighafi muhimu kwa mahitaji mengine ya mwanadamu. Dawa hizo huingia mwilini kwa njia kuu tatu: kunywa, kula na kunusa.

Ziko ambazo zimeruhusiwa kisheria kwa sababu maalum, ikiwamo matibabu. Pia, kuna tumbaku na pombe zinaruhusiwa, ila ina madhara, huku kuna visivyoruhusiwa, kama bhangi, mirungi, cocaine, heroin na mandrax.

Pia, hospitali kunatumika valium na pethidine.

Kwa mujibu wa taarifa za Uingereza, bhangi duniani inagusa matumizi zaidi ya watu milioni 296 mwaka 2021, ikiwa ongezeko la asilimia 23 katika miaka 10 iliyopita imeeleza ripoti hiyo ya Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayohusika na kupambana na dawa za kulevya na uhalifu, UNODC.

Takwimu mpya zinaweka makadirio ya kimataifa ya watu wanaojidunga dawa za kulevya kwa mwaka 2021 kuwa milioni 13.2, asilimia 18 juu kuliko ilivyokadiriwa hapo awali.

Ripoti hiyo inaeleza zaidi kwamba, idadi ya watu wanaougua matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya imepanda kufikia watu milioni 39.5, sawa na ongezeko la asilimia 45 katika kipindi cha miaka 10.

Aidha ripoti hiyo ya dunia ya dawa za kulevya pia inaangazia jinsi ukosefu wa usawa wa kijamii na kiuchumi unavyosukuma na pia unavyosukumwa na changamoto za dawa za kulevya.

Pia, kuna uuharibifu wa mazingira na ukiukwaji haki za binadamu, unaosababishwa na uchumi haramu wa dawa za kulevya na kuongezeka dawa za kulevya zinazotengenezwa viwandani.

Mahitaji ya kutibu magonjwa yanayohusiana na dawa za kulevya bado hayajafikiwa, ripoti hiyo ikieleza ni mtu mmoja tu kati ya watano wanaougua matatizo yanayohusiana na dawa za kulevya waliokuwa katika matibabu.

Matumizi ya dawa ya kulevya mwaka wa 2021 na tofauti zinazoongezeka katika upatikanaji wa matibabu katika maeneo yote ulimwenguni.

Vijana ndio wako hatarini zaidi kutumia dawa za kulevya, pia huathiriwa zaidi na magonjwa ya matumizi ya dawa duniani.

Barani Afrika inatajwa, asilimia 70 ya watu wanaopata matibabu dhidi ya dawa za kulevya wako chini ya umri wa miaka 35.

Hivyo, ripoti inaeshauri umma kupewa kinga, ifikie huduma za matibabu kwa kipaumbele duniani kote, vinginevyo dawa za kulevya zitabaki kuwaumiza wengi zaidi.

Pia kunasisitizwa zaidi, hitaji la hatua za utekelezaji sheria, ili kuendana na miundo ya kisasa ya biashara ya uhalifu na kuenea kwa dawa za kulevya za bei nafuu zinazotengenezwa viwandani na rahisi kufikishwa sokoni.

Akitoa maoni yake, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya UNODC inayohusika na dawa za kulevya nchini Marekani, Ghada Waly, akasema idadi wanaokabiliwa na shida ya kutumia dawa za kulevya duniani kote, huku matibabu yakishindwa kuwafikia wote wanaohitaji.

Tunahitaji kuongeza hatua dhidi ya makundi ya biashara ya dawa za kulevya yanayotumia mizozo na migogoro kimataifa, kupanua kilimo na uzalishaji haramu wa dawa za kulevya, hasa viwandani, ili kuchochea masoko haramu na yenye madhara makubwa.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, anaisihi jamii kutowatenga waathirika wa dawa za kulevya.

Hivyo, bila shaka mitindo mingine ya maisha tunayoiona ya kisasa wala aina manufaa mfano dawa matumizi ya dawa za kulevya, ujambazi na mapenzi ya jinsia moja jamii msifanye kitu kwa kuona mtandaoni, ni vyema kuchukuliwa hatua.

# RITA yamaliza mgogoro wa msikiti

**Na Kulwa Mzee**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini nchini (RITA), umeitaka Bodi mpya ya Wadhamini wa Msikiti wa Ijumaa, Mwanza, kujiepusha na ubadhirifu wa mali za msikiti sambamba na kuimarisha mshikamano miongoni mwa waumini.

Pia bodi hiyo imeagizwa kuacha kulipiza visasi kwa bodi ya wadhamini ya msikiti huo iliyovunjwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya ofisi kwa bodi mpya ya msikiti huo, Kabidhi Wasii Mkuu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Frank Kanyusi, uteuzi wa bodi hiyo mpya umetokea baada ya kuwapo kwa mgogoro uliodumu kwa zaidi ya miaka 30, baada ya kufanyika usajili wa mabadiliko ya katiba mwaka 1990.

"Sababu zinazotajwa kusababisha migogoro hiyo ni kutotambulika mabadiliko ya Katiba ya mwaka 1993 yaliyowasilishwa kwa Msajili Mkuu mwaka 1997, kutoelewana wajumbe wa bodi ya wadhamini iliyokuwapo, matumizi mabaya ya mali, fedha na kukosekana kwa uwazi katika taasisi," alisema Kanyusi.

Alisema Februari 2, mwaka huu, RITA iliunda kamati ya uchunguzi ambayo ilifanya kazi kwa kipindi cha mwezi mmoja na kukabidhi ripoti iliyoonesha kuna ubadhirifu wa takribani Sh. bilioni moja.

"Baada ya tuhuma zilizokuwa zikiikabili bodi iliyopita, niliunda kamati ya uchunguzi iliyowasilisha taarifa kwa mamlaka za uchunguzi (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU). Mpaka sasa kazi imeshaanza kufanyika na baadhi ya wajumbe wa bodi iliyopita wameshahojiwa.

Hivi punde TAKUKURU itakamilisha kazi yake na watakaobainika katika ubadhirifu huo taratibu za kisheria zitafuatwa ili kila mmoja apate stahiki kwa mujibu wa sheria." Alisema Kanyusi.

Kanyusi alitoa rai kwa wajumbe wa bodi mpya ya udhamini kutekeleza majukumu yao kama sheria inavyotaka na kusisitiza kuwa wao si wamiliki wa mali bali ni wasimamizi kwa niaba ya wanachama, hivyo wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Makamu Mwenyekiti Bodi Mpya ya Wadhamini ya Msikiti wa Ijumaa, Sherally Hussein, mbali na kuipongeza RITA kwa usimamizi mzuri, alisema wakati umefika wa kuunganisha nguvu kwa Waislamu wote wa msikiti huo ili usimamia malengo yaliyokusudiwa kuanzishwa kwa taasisi hiyo.

"Kwa sasa tuna imani kwani ile mivutano iliyotugawa kwa makundi tofauti tofauti imekwisha. Ni wakati sahihi sasa makundi yote kuungana ili taasisi yetu itoe mchango stahiki kwa waumini wote na taifa kwa ujumla wake," alisema Hussein.

Kanyusi aliahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa bodi mpya ya wadhamini katika uongozi ili iweze kutimiza majukumu yake kikamilifu kwa maslahi mapana ya waumini ya jumuiya ya Kiislam mkoa wa Mwanza.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph (wa pili kulia), akimpa maelezo Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Mathew Kundo (kulia), alipotembelea kisima cha maji kilichopo Kijiji cha Nala jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri: Kuna taasisi za umma zinatishia usalama wa nchi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameanika mambo yanayokabili sekta ya utumishi wa umma huku akitoa angalizo la kuwapo baadhi ya taasisi zinazotishia usalama wa nchi kutokana na kutofuata sheria na taratibu za utumishi.

Miongoni mwa mambo aliyotaja kutishia usalama ni moja ya taasisi kuwa na vibarua wengi kuliko waajiriwa huku zingine zikiwa na matumizi mabaya ya madaraka, ukatili wa kijinsia na kukataa kupokea waajiriwa wapya.

Akifungua kikao kazi cha Wakuu wa Idara za Rasilimaliwatu na Utawala katika Utumishi wa Umma kutoka kwenye wizara, wakala, mamlaka, mashirika na taasisi za serikali, juzi jijini hapa, Waziri Simbachawene alisema baadhi ya wakuu wa taasisi wanafanya majukumu yao ya kila siku kinyume cha kanuni zilizowekwa.

Alisema baadhi ya wakuu wa taasisi za umma wamekuwa wanakataa kuwapokea watumishi wapya wanaoajiriwa na wakati mwingine kuwahamisha kwa madai hawajashirikishwa.

"Wale mnaotoka kwenye taasisi, chukueni nafasi zenu mshauri vizuri wakubwa zenu. Zipo taasisi utafikiri si taasisi za nchi hii, yaani utafikiri za nchi nyingine, halafu utakuta mtu yupo pale taasisi ina utamaduni wa ajabu na tukipeleka maelekezo kwa mujibu wa sera na sheria hawazingatii na wengine wanabisha, wanasema 'haiwezekani!'

"Zipo taasisi kubwa hapa zinatishia usalama wa nchi na moja ya taasisi ambazo mimi kusema ukweli zinanikera kwa masuala ya kiutumishi na Katibu wa Tume upo hapa, mnapaswa kufanya tathmini ya masuala ya kiutumishi kwenye taasisi," aliagiza.

Waziri huyo alimwagiza Katibu Mkuu wa ofisi hiyo kutafuta fedha ili taasisi hizo zifanyiwe tathmini kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina ili kubaini kama wanazingatia masuala ya utumishi wa umma.

"Zipo taasisi zimekufa lakini unaona tu watu ni harakati tu zinaendelea, lakini hamna kitu, hamna mfumo, hamna nini halafu ni taasisi muhimu lakini kila anayeingia pale anaambiwa 'sikia utaratibu ni huu na utakaa miaka miwili', atateuliwa mkurugenzi mwingine.

"Ameingia rafiki yangu mmoja anaitwa Nyamu pale TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania), lile dubwasha lile lina vibarua kuliko hata walioajiriwa, hawana mfumo mzuri wa kuajiri watu kwa mikataba, yaani pale ni harakati," alisema.

Waziri Simbachawene alisema alishaongea na huyo rafiki yake na anajitahidi kuweka mambo licha ya kuonesha bado kuna tatizo.

"Zipo na taasisi nyingine sizitaji ila ninaitaja hii kwa sababu ni ya rafiki yangu na anajitahidi, anafanya kazi vizuri sana na ofisa utumishi tulimbadili pale tukapeleka dada mmoja, ninaona kimya siku hizi angalau, taasisi zingine sizitaji, kuna watu wengine wana nongwa," alisema.

Pamoja na hayo, Simbachawene alikemea tabia ya kukaimisha watu wasio na sifa kwenye vitengo na kwamba hata mwenye sifa hawataki kumkaimisha. Sasa wawakaimishe kwa kuwa serikali ni mali ya wote.

"Unajua mimi niliwahi kuwa kondakta wa basi moja. Kati ya falsafa nilizojifunza kwenye ukondakta wangu wa basi, ukitaka tajiri upate fedha, hakikisha dereva na kondakta wanagombana kila siku na kila mmoja akija, sema 'ninakuamini wewe, niletee taarifa zote'.

"Akitoka kondakta anaingia dereva, anasema 'angalia huyu anashika fedha atakuwa mwizi', kwahiyo watakuwa wanajichongea wewe, ndo unapata! Wakielewana wewe hupati kitu. Kwahiyo ukitaka kukaa na mtu unayeelewana, wakati mwingine watu wasipoelewana wanafanya kazi vizuri zaidi," alisema.

Alisema watu wakielewana sana wanasababisha kukosekana kwa ufanisi kwenye utendaji kazi.

"Ninawaelekeza kupitia kikao hiki kila mmoja kushughulikia changamoto zilizobainishwa kwenye kukaimisha nafasi pamoja na ujazaji nafasi hizo kwa wakati," aliagiza.

Aliwatahadharisha wasimamizi wa kazi ambao hawatekelezi majukumu yao ipasavyo. Watachukuliwa hatua.

Kuhusu Mfumo wa Tathmini ya Mahitaji ya Watumishi (HR Assessment), alisema taarifa zimebaini nafasi wazi 1,231 za wakuu wa idara na vitengo kuanzia kwenye wizara, idara zinazojitegemea, wakala wa serikali, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi za umma.

Pia alisema kuwa hadi kufikia Novemba 30 mwaka huu, ofisi hiyo ilipokea maombi ya kujazwa nafasi wazi za uongozi 1,286 na hadi sasa nafasi 835 sawa na asilimia 65 za uongozi zimeshajazwa.

Aliwaelekeza waajiri wote wahakikishe wanajiunga na kutumia kikamilifu mifumo ya kiutumishi na uwajibikaji ambayo imesanifiwa na ofisi hiyo na wasafishe taarifa za watumishi zilizopo katika Mfumo Jumuishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi) ili kusaidia kutoa uamuzi sahihi wa masuala mbalimbali ya kiutumishi.

Waziri huyo alisema kuwa kwa mwaka 2024/25, serikali imetoa kibali cha kuajiri watumishi 45,080 wa kada mbalimbali, wakiwamo 10,396 wa kada za afya na 10,590 wa kada za ualimu.

Naibu Waziri, Deus Sangu alisema pamoja na kazi inayofanywa na serikali, kumekuwapo na malalamiko kwa baadhi ya watumishi ambayo kwa kiasi kikubwa yanafanana na mengi ni ya muda mrefu na yapo katika dhamana ya waajiri kisheria, lakini hayashughulikiwi kwa wakati.

Awali, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Juma Mkomi alibainisha kuwa kikao kazi hiko kitajikita zaidi kujadili masuala mbalimbali ukiwamo usimamizi wa rasilimaliwatu na matumizi ya Tehama.

# Watuhumiwa hujuma SGR wapandishwa kizimbani

Na Mwandishi Wetu

WATUHUMIWA watano, wakiwamo raia wa kigeni wawili, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Kibaha na kusomewa mashtaka matano ya uhujumu wa mali za Shirika la Reli Tanzania (TRC) na kusababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. milion 200.

Hao ni Zhang Feng, Wang Yong, Paulo John, Abdul Mohamed na Pius Kitulya, wakazi wa Miwaleni Mlandizi.

Akisoma hati ya mashtaka, Mwendesha Mashtaka wa Serikali Joseph Kisaka alidai kuwa kati ya Novemba na Desemba mwaka huu, washtakiwa hao walikutwa na nyaya za reli ya kisasa (SGR) zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200.

Hata hivyo, washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza shauri hilo, isipokuwa panapokuwa na idhini maalumu ya Mahakama Kuu.

Baada ya kusomewa maelezo hayo, washtakiwa hao walirudishwa rumande na kesi yao imepangwa kutajwa Desemba 30, mwaka huu chini ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Kibaha, Felista Mweru.

**KESI YA DODOMA**

Mkoani Dodoma kesi namba 30205 ya mwaka 2024 inayomkabili mshtakiwa Said Masoud na wenzake wawili ya kudaiwa kufanya uharibifu wa miundombinu ya SGR na kuisababishia serikali hasara ya dola 5,415.8, imeahirishwa hadi Desemba 31 mwaka huu.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Dodoma, Denis Mpelembwa, aliahirisha kesi hiyo jana baada ya wakili wa upande wa serikali, Zubeda Lyami kudai kuwa upelelezi haujakamilika.

Wakili huyo alidai wa kesi hiyo ilikuja juzi kwa ajili ya kutajwa kwa mara kwanza, lakini kutokana na kutokamilika kwa upelelezi, anaomba ipangiwe tarehe nyingine.

Kabla ya hakimu hajataja tarehe nyingine ya kesi hiyo, mshtakiwa namba moja Said Masoud, alihoji sababu za kupungua kwa idadi ya washtakiwa, akidai kuwa awali walikamatwa washtakiwa wanne, lakini wakati wa kusomewa mashtaka, mmoja wao aliondolewa.

Hakimu Mpelembwa alimtaka Wakili wa Serikali Lyumi kutoa ufafanuzi kuhusu hoja hiyo; naye akadai jukumu la kufuta kesi ya mshukiwa ni la Mwendesha Mashtaka wa Serikali, hivyo wao hawajui vigezo vilivyochukuliwa kufuta mashtaka kwa mmoja wa waliowakamata awali.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Mpelembwa aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 31 mwaka huu itakapoanza kusikilizwa.

Novemba 11 mwaka huu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, akizungumza na waandishi wa habari, alidai kuwakamata watu sita kwa tuhuma za kuhujumu miundombinu ya SGR kwa kukata na kuiba nyaya za shaba kutoka katika madaraja matatu ya reli hiyo katika wilaya za Mpwapwa na Bahi.

Vilevile, Kamanda Katabazi siku hiyo alitangaza alichokiita "vita vya kuusaka na kuuteketeza mtandao mzima wa uharibifu wa miundombinu hiyo".

***Imeandaliwa na Julieth Mkireri (KIBAHA) na Paul Mabeja (DODOMA)**

# Dereva bodaboda anusurika, wenzake waenda jela maisha

## • Ni baada ya kukaa mahabusu miaka mitano

Na Kulwa Mzee

DEREVA bodaboda William Daraja amenusurika kwenda jela, huku abiria aliyembeba na mwenzake wakihukumiwa kutumikia kifungo cha maisha gerezani baada ya kupatikana na hatia ya kusafirisha gramu 983.5 za dawa za kulevya aina ya Heroine.

Bodaboda huyo aliyekaa mahabusu gerezani kwa miaka mitano, alinusurika kifungo cha maisha jela jana katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Sedikia Kisanya aliyesoma hukumu iliyowatia hatiani washtakiwa wawili kati ya watatu.

Washtakiwa waliotiwa hatiani na kupewa adhabu ya kifungo cha maisha jela ni Hassan Mohamedi na Hassan Hassan aliyekuwa abiria wa mshtakiwa wa tatu William.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Kisanya alisema washtakiwa kwa pamoja Septemba 4 mwaka 2019, Tegeta Pwani eneo la Nyaishozi, wilayani Kinondoni, walikutwa wakijihusisha na biashara ya kusafirisha dawa za kulevya, Heroine gramu 983.5.

Alisema Jamhuri katika shauri hilo iliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Tully Helela, akisaidiana na Wakili Eric Kamala. Waliita mashahidi sita na vielelezo 10.

Jaji Kisanya alisema upande wa utetezi ulikuwa na mashahidi wanne, wakiwamo washtakiwa watatu.

Alisema ushahidi wa upande wa mashtaka ulidaiwa Septemba 4, 2019, ASP Hassan Msangi, akiongoza askari wengine, walifanya ukaguzi katika maeneo yanayodhaniwa kufanya biashara ya dawa za kulevya. Wakiwa Madale walipata taarifa kutoka kwa msiri kwamba maeneo ya Tegeta Nyaishozi kulikuwa na watuhumiwa.

Ilidaiwa walielekezwa eneo la tukio, wakaenda na walipofika, muda mfupi mshtakiwa Hassan Aziz Mohamed alifika eneo hilo akifuatwa na mshtakiwa wa pili Hassan Hassan ambaye alifika na bodaboda iliyokuwa inaendeshwa na William Daraja.

Ilidaiwa katika ushahidi kwamba washtakiwa wote watatu waliwekwa chini ya ulinzi, walitafutwa mashahidi wa kushuhudia upekuzi, walipofika upekuzi ulifanyika, likapatikana begi la rangi ya kijani ndani kulikuwa na mfuko wa mweusi wa plastiki uliobandikwa nembo inayosomeka 'Farmer Cashew Kernels' ndani yake ukiwa na unga.

Katika upekuzi, mshtakiwa wa kwanza alikutwa na pochi nyeusi, fedha taslimu Sh. 150,000, Dola za Marekani 77, fedha za Afrika Kusini Randi 900, leseni ya gari na simu ya mkononi.

Baada ya upekuzi ilidaiwa waliandaa hati ya kukamata mali. Septemba 6, 2019 walifunga kielelezo kwa ajili ya kupeleka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchunguzi, unga ulipimwa ikabainika ni gramu 983.5 na sampuli ilipofanyiwa uchunguzi ilibainika ni Heroine.

Washtakiwa ilidaiwa walijitetea kwa kukana kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya, mshtakiwa wa kwanza alidai alikamatwa eneo la DAWASCO Tegeta, mshtakiwa wa pili alipofika kujua sababu naye alikamatwa na mshtakiwa wa tatu alipofuata malipo kwa abiria wake, mshtakiwa wa pili alikamatwa pia.

Mshtakiwa wa pili alidai alilazimishwa kutia saini maelezo ya onyo na mshtakiwa wa tatu William alidai ni dereva bodaboda, alikodiwa maeneo ya Tegeta Nyuki na mshtakiwa wa pili ampeleke DAWASCO na alifanya hivyo.

Alidai alipomfikisha alikuta askari, alipofuata malipo yake kwa mshtakiwa wa pili naye akakamatwa akaunganishwa na mshtakiwa wa kwanza na wa pili katika tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya.

Jaji Kisanya alisema mahakama baada ya kupitia ushahidi iliona hakuna ubishi kwamba washtakiwa wote watatu walikamatwa na shahidi wa tatu wa upande wa mashtaka akishirikiana na askari wengine.

Alisema ni wazi kwamba washtakiwa wote si wakazi wa Tegeta, maeneo la DAWASCO na Nyaishozi yako Mtaa wa Tegeta Pwani iliko Ofisi ya Serikali ya Mtaa.

"Ni wazi kwamba hayo maeneo mawili yako karibu, ushahidi uliotolewa dhidi ya mshtakiwa wa tatu ni kwamba hakuna ubishi kuwa William ni dereva wa bodaboda alimwendesha mshtakiwa wa pili Hassan.

"Upande wa Jamhuri umeshindwa kuleta ushahidi wa kuthibitisha kwamba bodaboda haikuwa imesajiliwa kufanya kazi hiyo na madai ya mshtakiwa wa tatu kwamba mshtakiwa wa pili alikuwa abiria wake.

"Upande wa mashtaka ulitakiwa kuleta ushahidi wa kuonesha bodaboda huyo alikuwa anajua kuhusu dawa za kulevya alizobeba abiria wake kwenye begi la kijani, ushahidi huo haukuletwa," alisema Jaji Kisanya.

Alisema kutokana na ushahidi, mshtakiwa wa kwanza na mshtakiwa wa pili wanahusika na biashara ya dawa za kulevya na kwamba washtakiwa walilalamika katika ushahidi wao lakini hawakuhoji maswali mashahidi wa upande wa mashtaka wakati wakitoa ushahidi wao mahakamani.

"Mahakama imezingatia ushahidi wa pande zote mbili, upande wa mashtaka umethibitisha kosa bila kuacha shaka, inawatia hatiani mshtakiwa Hassan Mohamedi na Hassan Hassan kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya.

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwenga Tower Building-Kijitonyama
NewBagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dares Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4677
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | NELOYT(T) LIMITED | GARI | T950 DTG - MAN' TGX 24440 | GSP AUCTION MART | 30/12/2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

ANGEL ADAM KITOMARI

anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 874 CUM.** Chassis Namba **MD2B15BX5LWJ88121,**Engine Namba **JVXWLJ15716**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi namba

**:PHQ/ARU/ARU/48488/2024**

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

GODFREY MARTIN SHAURI

Anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya SUZUKI SCUDO yenye Usajili T 705 ATR, Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu nae.

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/TAN/LUSH/13753/2024**



# TCB yapeleka mashindano ya kahawa kimataifa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BODI ya Kahawa Nchini (TCB) na Chama cha Kahawa Bora Afrika (AFCA) wamepeleka mashindano ya ubora wa kahawa ya nchini ngazi ya kimataifa ili kuwawezesha wakulima nchini kushindana na wazalishaji wa zao hilo wa nchi nyingine.

Jana Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Kajiru Kisenge, ambaye ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kahawa, alisema kuwa African Fine Coffees Association (AFCA), imejitosa kuongeza kuitangaza kahawa ya Tanzania ili kuwapa fursa wakulima wadogo waliounganishwa kwenye vikundi, Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) kushindana kimataifa na wazalishaji wakubwa duniani.

Mashindano hayo yanaongozwa na Jaji, Grace Mukayisenga kutoka nchini Rwanda, yanawashirikisha majaji wengine, Herman Kusaga (Kilikafee, D and J Distributors Co. Ltd), Eliaringa Macha (Burka Cofee Estates Ltd) na Frank Mlay (Tanzania Coffee Board) na Philipina Saritha (African Plantations Kilimanjaro Limited).

"Kwa hiyo Bodi ya Kahawa, tunafanya kila mwaka na mwaka huu mashindano haya yanafanyika makubwa zaidi kwa sababu ya ushirikiano na Chama cha Kahawa Bora Afrika (AFCA)," alisema na kuongeza kuwa: "Tumeamua kuipeleka kahawa yetu ngazi ya kimataifa ili kahawa yetu iweze kushindana na kahawa za wazalishaji wa nchi nyingine.

Alisema madhumuni ya mashindano haya ni kuhamasisha wakulima wa kahawa kuzalisha yenye ubora na kuzingatia kanuni bora za kilimo hicho.

"Ubora wa kahawa ndio kila kitu kuwawezesha wakulima kupata bei nzuri na kujenga brand ya kahawa yake (chapa)," alisema.

Ofisa Masoko Mwandamizi wa TCB na Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Ubora, Naishoki Lukumay, alisema mashindano hayo yanahusisha sampuli 77, kati ya hizo, wakulima wakubwa wamewasilisha 18, vyama vya msingi na vikuu 58.

Lukumay, alisema mashindano hayo ya tano, yanafanyika makao makuu ya TCB mjini Moshi Mkoa wa Kilimanjaro kuanzia Desemba 16 hadi 20 mwaka huu.

Alisema mashindano hayo yana tija kwa sababu kuna sampuli nyingi kutoka sehemu tofauti zinazolima kahawa nchini.

Abertus Paschal, mkulima kutoka Chama Kikuu cha Ushirika cha Kagera (KDCU), alisema wamewasilisha sampuli za kahawa yao ili kuona ubora kuanzia mnyororo wa thamani, hasa kwenye uzalishaji, uvunaji, kuiandaa na kukoboa.

"Matokeo yakitoka ni chachu kwa sisi wakulima kutambua tumekosea pahala fulani, tuweze kusahihisha," alisema.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko (wa pili kushoto), Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande (wa tatu kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda (kushoto), wakitembelea mabanda mbalimbali ya maonesho katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano (AICC), kabla ya kufungua Kongamano la 15 la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataalamu ugavi wahimizwa kuzingatia maadili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amewataka wataalamu wa ununuzi na ugavi nchini kizingatia maadili ili kuiwezesha serikali kuleta maendeleo kwa wananchi.

Dk. Biteko alisema hayo jana jijini Arusha wakati akifungua kongamano la 15 la wataalamu hao jijini hapo.

Alisema wataalamu hao ni muhimu kuchagiza maendeleo na serikali inawategemea kufanikisha mipango yake.

"Wataalamu wa manunuzi na ugavi mna mchango mkubwa zaidi ya asilimia 70 ya bajeti nzima kwa manunuzi, kuweni waadilifu, chukueni rushwa na kushauri namna bora ya kufanikisha mipango ya maendeleo.

"Kutokana na ukubwa wa majukumu yenu, kuna uwezekano rushwa kubwa ikapita mikononi mwenu, majadiliano haya yawawezeshe kuzuia na kukabiliana na vitendo hivi," alisema.

Biteko, alisema ni wajibu wa wataalamu hao kulinda taaluma yao ili isiingiliwe na watu wasiokuwa na sifa zinazohitajika.

Alizitaka mamlaka husika kuwatambua na kuwapa motisha wataalamu wenye sifa kwa mujibu wa sheria.

Vilevile, aliwataka washiriki wa kongamano hilo kujifanyia tathmini utendaji wao wa kazi ili kuondokana na changamoto zinazoweza kuichafua taaluma ya ununuzi na ugavi.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande aliwataka washiriki hao kufanya kazi zao kwa kushirikiana na kuahidi wizara yake inaendelea kutafuta suluhisho la changamoto zinazowakabili.

Chande, alitaja miongoni mwa mambo yanayosababisha serikali kukwama katika mipango yake kuwa ni wivu, choyo na fitna baina ya watumishi.

Alishauri watumishi hao kuachana na vitendo hivyo kwa sababu vinakwamisha maendeleo nchini.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Benezeth Ruta, aliishukuru serikali kwa kutenga fedha kuwezesha taaluma hiyo kusonga mbele.

## Serikali yawaangukia wadau ajira kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

SERIKALI mkoani hapa, imewataka wadau na wapenda maendeleo kuelekeza nguvu zao kupambana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana katika Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilida Burian, wakati akizindua Jukwaa la Vijana Wilaya ya Tanga katika viwanja vya shule ya kimataifa ya Tanga wiki iliyopita.

Balozi Batilida alisema ametoa rai hiyo ili kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana kuwa bado ni changamoto inayoikabili halmashauri hiyo na nyingine mkoani humo.

Alisema hawana budi kupambana nayo kwa nguvu zote na changamoto hiyo kwa kuihusisha serikali ya mkoa huo.

Kwa mujibu wa Batilda, sensa iliyofanywa na Taasisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), imeonesha bado changamoto ya ajira kwa vijana ni kubwa, hivyo kila mmoja anatakiwa kuchukua hatua, wakiwamo vijana wenyewe kukabiliana nayo.

Kwa mujibu wa sensa hiyo, kati ya vijana147,000 wenye umri wa miaka 15-30 katika jiji hilo, 109,000 wameajiriwa sekta rasmi na sizizo rasmi huku wengine takriban 5,000 wakiendelea kutafuta kazi.

Alisema serikali inatambua changamoto hiyo ya ajira kwa vijana na kuchukua hatua kuweka mazingira wezeshi kwa wadau wa ndani na nje nchi kuendeleza kundi hilo.

Alisema serikali pia imefanya mapitio ya sera ya vijana na kutengeneza sera nyingine kusaidia kuchangisha upatikanaji wa ajira kwa vijana kwa kuajiriwa na kujiajiri.

Mkuu huyo wa mkoa, alisema jiji hilo limekuwa mstari wa mbele kuhakikisha vijana wanatumia fursa zilizopo katika maeneo yao kupata ajira.

Aliyataja mambo yanayopaswa kufanyika kukabiliana na tatizo hilo kuwa ni kuweka mazingira mazuri ya wadau kufanya kazi katika jiji hilo.

Balozi Batilda alipongeza Mradi wa Tanga Yetu kwa kushirikiana na halmashauri hiyo na baadhi ya viongozi wa serikali kupambana na tatizo la ajira kwa vijana wa jiji hilo kwa kuzalisha miradi katika sekta za uzalishaji mali na kunufaisha kundi hilo kwa kuajiriwa na kujiajiri.

Vilevile, aliwahimiza vijana katika jiji hilo wasiokuwa na ajira kuchangamkia fursa zinazotolewa na Tanga Yetu na kuondokana na umaskini badala ya kutumia muda mwingi kukaa vijiweni kupiga porojo.





# Mume amkata mkewe mkono, kisa wivu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Shinyanga linamsaka Mkazi wa Kata ya Mwendakulima Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kwa tuhuma za kumkata mkewe, Happyness Khalfan (30) mkono wa kushoto kwa kinachodaiwa wivu kwa kuchelewa kurudi nyumbani.

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Janeth Magomi, amethitibisha kutokea kwa tukio hilo Desemba 15, mwaka huu na kusema jeshi hilo bado linaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini chanzo chake.

Kamanda Magomi, alisema tukio hilo liliripotiwa na baadhi ya jirani wa wanandoa hao baada ya majeruhi huyo kufanya siri.

"Baada ya mtuhumiwa kumkata mkono mkewe alikimbilia kusikojulikana, tunamsaka, akikamatwa atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka," alisema Magomi.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Vicent Ndesekio, alilaani kitendo hicho huku akiiasa jamii kuacha kujichukulia sheria mkononi na kufuata taratibu za utatuzi wa migogoro inapojitokeza katika maeneo yao.

Ofisa Kliniki Mwandamizi wa Kituo cha Afya cha Mwendakulima, Leonard Mabula, alithibitisha kumpokea majeruhi huyo na kuanza kumpatia matibabu.

Mabula, alisema Happyness, amejeruhiwa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali mkono wake wa kushoto na kwamba alipofikishwa kituoni alikuwa akivuja damu nyingi.

Alisema hali yake inaendelea vizuri, endapo itabadilika na kuwa mbaya, atapatiwa rufani kwenda Hospitali ya Wilaya Kahama kisha Hospitali ya Kanda ya Bugando jijini Mwanza kwa matibabu zaidi.

Akizungumzia tukio hilo, Happyness, alisema lilitokea baada ya kuchelewa kurudi nyumbani na kumkuta mumewe akiwa na hasira.

Alisema kitendo hicho kilisababisha kuzuka ugomvi baina yao na kujeruhiwa kwa kukatwa mkono huo na kitu chenye ncha kali.

Alisema mumewe huyo aliamuru mkewe huyo asipelekwe hospitali kwa kuhofia kukamatwa na polisi na kutaka tukio hilo iwe siri ili aweze kutibiwa kwa dawa za asili.

Alisema kutokana na maumivu makali, jirani walimsikia alivyokuwa akilalamika na kutoa taarifa kwenye vyombo vya sheria katika maeneo yao.

Alisema baadaye alichukuliwa na kupelekwa katika kituo hicho cha afya kwa matibabu.



Umati wa watu wakitoka na wengine kuingia katika kituo cha daladala za kuelekea Segerea kilichopo Mbezi Mwisho Dar es Salaam jana. Kituo hicho kwa sasa kimezidiwa na wingi wa daladala, bajaj, bodaboda na wafanyabiashara. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Tabora mpya sasa kuwa ya kisasa

**Na Halima Ikunji,** TABORA

ZAIDI ya Sh.bilioni 19 zimetolewa na Benki ya Duniani (WB) kwa ajili ya kubadili mandhari ya maeneo ya Manispaa ya Tabora kuwa ya kisasa ya soko kuu, stendi na barabara kuweka lami.

Akizungumza na Nipashe Meya wa Manispaa hiyo, Ramadhan Shabani Kapela, alisema maandalizi ya ujenzi wa miradi hiyo na kuwa ya kisasa chini ya Mradi wa TACTIC yamekamilika.

Kapela, alisema makandarasi wamepatikana na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi ujao.

Alisema barabara za lami zenye urefu wa kilomita 0.7 zimeanza kujengwa katika baadhi ya mitaa ya manispaa hiyo.

Kwa upande wa ujenzi wa soko hilo kutoka la zamani na kuwa la kisasa, alisema kinachosubiriwa ni baadhi ya wafanyabiashara kuhama na kumpisha mkandarasi kuanza kazi.

"Wafanyabiashara wote wa soko kuu walishirikishwa katika hatua zote kwenye maandalizi ya utekelezwaji mradi huo na walipewa muda wa kutosha kujiandaa kuhama kupisha utekelezwaji mradi huo," alisema Kapela.

Aliwataka wafanyabiashara kuondoka kabla ya Januari 1, mwakani ili kumpisha mkandarasi kuanza kazi ya ujenzi wa mradi huo.

Alisema wafanyabiashara hao wanatakiwa kuondoka kwenye soko hilo na kwenda kwenye maeneo ambayo wametengewa kuendesha shughuli zao kwa muda.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Manispaa hiyo, Shaban Malunda, alisema wako tayari kumpisha mkandarasi kuanze kazi yake na kuahidi kutoa ushirikiano wa kutosha.

Malunda, aliomba ujenzi wa mradi huo utakapokamilika, kila mfanyabiashara apate nafasi pasipo usumbufu wowote.

# Jela maisha kwa kulawiti mdogo wake

**Na Vitus Audax,** KWIMBA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Kwimba imemuhukumu kifungo cha maisha jela, Ng'oga Mashauri (20), Mkazi wa Kitongoji cha Mwankuba Kijiji cha Nyambiti baada ya kukutwa na hatia ya kumlawiti mdogo wake mwenye umri wa miaka minne.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, John Jagadi baada ya ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka kuthibitisha bila kuacha shaka kuwa mshtakiwa huyo alimlawiti mtoto huyo wa baba yake mdogo.

Awali Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Juma Kiparo, alidai kuwa Oktoba 27, mwaka huu katika kijiji hicho, mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Alidai mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani hapo Novemba 11, mwaka huu na kusomewa shtaka hilo.

Alidai mashahidi wakiwamo wawili, mtoto huyo na mzazi wake na wengine wa mashtaka walitoa ushahidi dhidi ya mshtakiwa huyo na kutiwa hatiani.

Baada ya mahakama hiyo kusikiliza mashahidi hao, Hakimu Jagadi, alisema ushahidi wao umethibitisha bila kuacha shaka kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Jagadi alimpa nafasi ya kujitetea mshtakiwa huyo, ambapo aliiomba mahakama hiyo kumwachia huru kwa madai kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza.

Mwendesha Mashtaka huyo alipinga utetezi huo na kuiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi yake kwa madai kuwa kitendo alichomfanyia mdogo wake huyo ni ukatili uliopitiliza.

Hakimu huyo alikubaliana ombi hilo huku akinukuu vifungo vilivyotolewa vya sheria vilisomwa mahakamani hapo na mwendesha mashtaka huyo na kumhukumu kifungo cha maisha jela.

# Shy wajihami kwa ukame

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MITI ya kivuli katika baadhi ya maeneo mkoani hapa iko hatarini kukauka kutokana na ukame uliosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Uchunguzi umebaini kuwa miti hiyo ni ile iliyopandwa katika kampeni mbalimbali ili kutunza na kukabiliana na uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji miti ovyo kwa shughuli za binadamu.

Taasisi za umma ikiwamo Chuo cha Sayansi za Afya Kolandoto, ni miongoni mwa maeneo ambayo miti yake imeanza kukauka kutokana na hali hiyo.

Katika chuo hicho, inadaiwa kuwa licha ya athari hizo kusababisha uharibifu wa mazingira pia kunasababisha ukosefu wa kivuli kwa ajili ya wanachuo na watu mbalimbali kupumzika na kujisomea.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Mipango, Fedha na Utawala, Michael Henerikо, aliliambia Nipashe juzi wameanza mkakati wa kurejesha miti hiyo katika hali ya awali ya ustawi.

"Kuna baadhi ya maeneo yameathiriwa hasa sehemu ya mbele ya jengo la utawala na sasa tupo kwenye harakati za kuweka kifusi ili kusawazisha na kutengeneza bustani," alisema.

Msimamizi wa Mazingira chuoni hapo, Josephine Charles, alisema wamekwisha anzisha kampeni ya kuhifadhi mazingira katika maeneo hayo.

Josephine, alisema kuanzia Aprili hadi Desemba 10, mwaka huu wamepanda miti zaidi ya 700 na kuandaa vitalu vya miche.

Mwanafunzi wa chuo hicho, Magreth Milimo, alisema kukithiri kwa ukame kunaathiri wanafunzi kwa kusoma katika mazingira ambayo siyo rafiki, ikiwamo kukosa vivuli na joto kali.

Akizindua kampeni ya kupanda miti, Mkuu wa Wilaya hiyo, Julius Mtatiro, aliagiza kila kaya kupanda miti kwenye maeneo yao ili kutunza mazingira.

Kwa upande wa taasisi za serikali hususan, shule alimtaka kila mwaka mwanafunzi kupanda mti na kuutunza.

Ofisa Misitu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anjela Erasnus, alisema katika kampeni hiyo, halmashauri ya manispaa na wilaya ya Shinyanga hadi kufikia Mei mwakani kila moja inatakiwa kupanda miti milioni 1.5.

ama
ALHAMISI DESEMBA 19, 2024
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

## WAJIKI, Polisi wanavyokoleza moto kampeni maalum vita ukatili kijinsia




## Shuleni Kawe 'A' kunavyokabiliana na joto kali, kuwahudumia maji wanafunzi

Ukurasa 13

### SIKU 12 ZIKISALIA KUUAGA 2024

# Bima Toto Afya inavyomkamilishia Samia mkanda kuwajibika jamii kiuzazi

•Atoa mfukoni mwake: Tiba, kusomesha, ajenga nyumba, mitaji...

**Na Mwandishi Wetu**

MOJA ya wasifu ambao Rais Dk. Samia Rais amekuwa akijinadi nao kiutawala, kisiasa na wanajamii, ni katika nafasi yake kijinsia kama mama na anawajibika katika wasifu huo.

Kadri akifuatiliwa matendo yake kiutawala, huangukia katika wajihi huo kuanzia nasaha zake, matendo hadi utekelezaji.

Ikiangaliwa kwa kina nyendo hizo, kuna nafasi ya uzazi, mahususi kiafya. Mwaka huu ukihitimu kuna hoja na vielelezo vingi katika ngazi ya utekelezaji kiafya, mbali na ujenzi wa majengo ya vituo vya afya na hospitali, vifaa na kuelimisha wataalamu.

Ni utendaji unaopata urafiki kutoka kwa mtangulizi wake, Dk. Jakaya Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne na mstaafu pekee aliye hai katika nchi na watano waliomtangulia Dk.Samia.

Dk. Kikwete katika afya, ana wasifu na rekodi kuwa mwasisi wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) uliobuniwa mwaka 2007 na kuanza kufanya kazi 2008.

Kwa sasa, mstaafu Dk. Kikwete ni Mjumbe wa Bodi ya Menejimenti nchini ya tawi la shirika la kiafya kimataifa, Nutrition International (NI), akiwa na mchango wa kuwezesha nyendo hizo, ikifaidisha utawala wa Rais Dk. Samia.

Mnamo Machi mwaka huu, ikaipatia Wizara Afya vidonge vya matone ya Vitamini A milioni 22, kwa ajili ya kuwapatie watoto walio




Waziri wa Afya, Jenister Mhagama, akiwa katika tukio la kurejeshwa Bima ya Afya nchini, katika utaratibu mpya aliyoutangaza wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

na umri chini ya miaka mitano, ziwafikie jumla yao milioni 11 kwa ajili ya kuwaongezea kinga ya mwili na kuimarisha afya yao ya macho.

Naibu Waziri wa Afya Godwin Mollel, ambaye kitaaluma ni tabibu wa binadamu, akahimiza: "Wazazi zingatieni lishe bora kwa watoto tangu wa utangaji wa mimba na kuwa na desturi ya kula mlo bora kwa mama wajawazito.

"Hii itamsaidia mtoto hata baada ya kuzaliwa na wakati yuko shule ubongo na akili yake kufanya kazi kikamilifu, pia itamkinga na magonjwa ya mara kwa mara," anasema Dk. Mollel.

Pia, Dk. Mollel anafafanua kuwa, pia Rais Dk. Samia ameelekeza fedha shilingi. bilioni 99 za kuajiri na posho za wahudumu wa afya ngazi ya jamii, ambao wamekuwa msaada mkubwa wa kufikisha elimu ya lishe na afya bora.

**ATIBU NA KUSOMESHA**

Hilo linatokea, huku Rais Dk. Samia katika uzazi wake huo, mnamo Februari, mwezi mmoja kabla ya kupokea dawa hizo za msaada, aliahidi kumsomesha mtoto Alhaji Abdallah (10) na wadogo zake watano.

Ni uamuzi wake, baada ya kutaarifiwa mtoto huyo kuacha shule akiwa darasa la tatu, kutokana na ugumu wa maisha na kulazimika kuuza ndizi, ili kuisaidia familia yake ya watu sita.

Hapo akaahidi kumpatia kiwanja na kumjengea nyumba mama yao, Ester Hussein, aliyekuwa mgonjwa.

Ni tukio la mkoani Kigoma, pale mtoto Alhaji aliomba kipaza sauti katika mkutano wa aliyekuwa Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, kuwasilisha kero yake, akiomba awezeshwe kupata elimu kwa kuwa mama yake hana uwezo akiumwa maradhi ya kuvimba tumbo.

Makonda baada ya kumsikiliza, alimwahidi CCM ingemsomesha na akaanzisha mchango wa papo kwa hapo kumsaidia, ikapatikana shilingi milioni 2.22.

Siku iliyofuata, Makonda akaenda kuitembelea familia hiyo na kumpatia ujumbe wa Rais Dk. Samia kuwasaidia familia hiyo watoto wote watano na kulipia vifaa vyote vya shule na sare.

"Rais Samia ameguswa na maisha ya Alhaji, ameona upendo aliona namna alivyokuwa anapigania maisha ya mama yake na wadogo zake na kipaji chake ya biashara, kwa sababu alikuwa anatunza fedha kutoka Sh. 4,000 hadi kufikia Sh. 20,000," akasema.

Akafafanua, Rais Dk.Samia ameamtuma kumfahamisha Alhaji, kwamba watajengewa nyumba ya kifamilia na ingekamilika ndani ya mwaka huu.

Kwa mujibu wa Makonda, ni jozi inayokamilika kwa kuwekwa vifaa kama viti, meza na vitanda na mama huyo kupata mtaji wa biashara shilingi milioni tano na kugharamia matibabu, akihakikishiwa kufanyiwa uchunguzi sahihi.

**OFA TIBA 100 KWA MPIGO**

Iikiwa kama nyendo zake za kawaida mnamo Aprili mwaka huu, mara nyingine akatoa ofa kudhamini tiba ya wagonjwa 100 wanaosumbuliwa na tatizo la mgongo wazi.

Kwa mujibu wa aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, mgongo wazi na kichwa kikubwa, ni tatizo linalowapata watoto, chanzo kikiwa ukosefu wa madini ya foliki asidi.

Akitoa ufafanuzi mjini Dar es Salaam, Waziri Ummy akatamka: "Rais Samia amenielekeza nilete pesa kwa ajili ya watoto 100, ambao wangefanyiwa upasuaji wa kichwa kikubwa na mgongo wazi bure kwa gharama zake.

"Kwa hiyo, Profesa (Abel) Makubi (Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma). Wasiliana na Chama cha Wazazi na Walezi wa Watoto Wenye Vichwa Vikubwa na Mgongo Wazi Tanzania, kujua watoto hawa ndani ya wiki moja, mbili Wizara italeta hizo fedha." Ni katika picha hiyo ya kile kinachojiri mwaka huu, suala la uamuzi kuhusu bima ya afya kwa watoto, ni mwendelezo wa mengi ya uzazi na ulezi kutoka kwa Rais Dk. Samia, ikiwa ni zaidi ya majukumu yake ya kawaida.

AFYA

# WAJIKI, Polisi wanavyokoleza moto kampeni maalum vita ukatili kijinsia

## •Wataja mzizi wa kikwazo ulikojificha




WAJIKI wakiwa katika maadhimisho hayo. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**NA SABATO KASIKA**

VITENDO vya ukatili wa kijinsia ni moja ya changamoto inayoendelea kutesa ndani ya jamii. Katikati ya vitendo hivyo, wapo wadau wanaoendelea kupambana navyo kupitia kampeni maalum.

Baadhi ya wadau ni Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), linaloendesha kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana'.

Wakati WAJIKI wakiendesha kampeni hiyo, Jeshi la Polisi nalo limekuja na kampeni iitwayo 'Tumwambie Kabla Hajaharibiwa'. Kampeni hizo zote zinalenga kukomesha vitendo vya ukatili ndani ya jamii.

Hivi karibuni kwenye maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, wadau hao waliungana kufanya maandamano wakiwa na mabango ya kuelezea madhara ya vitendo hivyo.

Siku ya kwanza, WAJIKI waliungana na Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Ilala, kisha siku ya pili wakaungana na Polisi Mkoa wa Kinondoni Dar es Salaam, kuendelea na maadhimisho hayo, huku wakuu wa polisi wa mikoa wakitoa taarifa kuhusu vita hiyo, mafanikio na changamoto zake.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ilala, ACP Yuston Mgonja, anasema kuanzia Januari hadi Desemba mwaka huu, watu 25 wamehukumiwa kwa makosa mbalimbali, mengi yakiwa ni ya ubakaji.

ACP Mgonja anafafanua kuwa, makosa ya ukatili katika kipindi cha mwaka 2024 yamepungua ikilinganishwa na mwaka jana na kwamba makosa ya ubakaji yako juu kuliko mengine.

"Mwaka jana makosa ya ubakaji yalikuwa 198, mwaka huu ni 77 ingawa bado yako juu kuliko mengine. Makosa ya ulawiti yalikuwa 87 lakini mwaka huu ni 51, makosa kipigo yalikuwa 79, mwaka huu ni 30, makosa ya kutelekeza familia yalikuwa 57, lakini mwaka huu ni 23," anasema.

Kamanda huyo anaongeza kuwa watu 25 wamehukumiwa vifungo vya miaka 30 na wengine. Maisha baada ya kukutwa na makosa mbalimbali, ina mengi ni ya ubakaji na ulawiti.

Wakati Ilala wakifungwa watu 25, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, SACP Mtatiro Kitinkwi, anasema katika mkoa wake kuna watu 25 wametumikia kifungo aina hiyo.

"Taarifa hii ni kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu. Vitendo vya ukatili wa kijinsia vipo, ndio maana tumepata idadi hiyo, hivyo tuendelee kushirikiana katika vita hii," anasema SACP Kitinkwi.

### CHANGAMOTO ZILIVYO

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ilala, ACP Mgonja, anasema pamoja na mafanikio ambayo jeshi hilo limepata kupitia kampeni ya 'Tumwambie Kabla Hajaharibiwa', bado kuna changamoto zinazotakiwa kutatuliwa.

"Jeshi la Polisi limekuwa likiendesha kampeni kwa kutoa elimu ndani ya jamii kwa kushirikiana na viongozi wa maeneo husika, shuleni.

"Katika vijiwe vya bodaboda na kwingine, lakini bado kuna watu hawatoi ushirikiano wanapoitwa mahakamani kutoa ushahidi," anasema.

ACP Mgonja anataja kikwazo kingine kuwa ni watu kutofika kwa wakati katika vituo vya polisi kutoa taarifa wanapofanyiwa ukatili na kusababisha ushahidi kuvurugika.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Mtatiro Kitinkwi, akiwa katika tukio hilo.

"Changamoto nyingine, ni baadhi ya wazazi na walezi kumalizana na wahalifu vinapotokea vitendo vya ukatili, lakini wanapopishana kiswahili ndipo wanapokuja kutoa taarifa wakati muda umeshapita na kusababisha ukusanyaji wa taarifa kuwa mgumu," anasema.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, anaunga mkono kauli ya kamanda huyo kwa kusema kuwa hata shirika lake katika vita hiyo limekumbana na vikwazo vya kukosa ushirikiano toka kwa jamii.

"Watu wanalalamika watoto wao kufanyiwa ukatili, lakini taarifa za matukio hayo zinapokusanya na kufikishwa polisi na kisha mahakamani, hawafiki kutoa ushahidi," anasema Janeth.

### SAFARI SALAMA

Mkurugenzi huyo anasema kwa muda mrefu, WAJIKI imekuwa ikiendesha kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana' katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke.

Anasema, kampeni hiyo inashirikisha madereva wa bodaboda, bajaji, daladala, viongozi wa serikali za mitaa, manispaa, TAKUKURU, walimu, wanafunzi na jamii, ikilenga kukomesha rushwa ya ngono kwa wanafunzi na wanawake.

"Ushirikiano huu na vyombo vya dola ni ishara tosha kuwa vita dhidi ya ukatili wa kijinsia inazidi kupamba moto. Sisi tunapiga vita rushwa ya ngono ambayo kimsingi ni ukatili wa kijinsia," anasema Janeth.

Anafafanua kuwa, hivi karibuni walizindua awamu ya sita ya kampeni hiyo eneo la Bunju 'A' Dar es Salaam, ili kuwajengea wanafunzi uelewa kuhusu madhara ya rushwa ya ngono itakayofikia wanafunzi 100,000.

"Women Fund Tanzania Trust (WFT-T), wametufadhili katika kampeni hii kwa kutupa Sh. milioni 80 ambazo tutazitumia kuokoa afya za Watanzania kwa miaka miwili," anasema.

Anafafanua kwamba walishamaliza kampeni katika Kata ya Bunju A na sasa wanaendelea na kata nyingine mpya, walizokuwa hawajazifikia za Kitunda wilayani Ilala na Mbagala Kibonde Maji, wilaya ya Temeke.

Anafafanua kuwa katika kampeni yao hiyo inayotarajia kudumu kwa miaka miwili, kila kata watafikia wanafunzi 35,000, walimu 100 na madereva 200 na kuwapa elimu ili wajue umuhimu wa kumlinda mtoto wa kike dhidi ya rushwa ya ngono.

Mkurugenzi huyo anaongeza kuwa mbali na kutoa elimu ya kupambana na rushwa ya ngono, wanahamasisha wanawake ili wajiandae kujitokeza kwa wingi kuwania uongozi katika uchaguzi wa mwaka 2025.

MAZINGIRA

# Shuleni Kawe 'A' kunavyokabiliana na joto kali, kuwahudumia maji wanafunzi

• Mikakati ya Klabu Mazingira, operesheni miti

**Na Grace Mwakalinga**

MTU anapofika katika Shule ya Msingi Kawe 'A', iliyoko Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam, kumejengwa mifumo na miundombinu inayoiwezesha kupata zaidi ya lita 6,000 maji kila siku.

Hiyo ni kwa ajili ya ya wanafunzi, walimu na wafanyakazi wengine mahali hapo, kukiwa kumejumuishwa matangi manne, yote kwa pamoja yana ujazo wa lita 1,000 zinazokidhi mahitaji ya wanafunzi zaidi ya 1,200 shuleni.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Cuthbert Mfwangawo, anasema lita hizo 1,000 za maji ya kunywa kutoka Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), hujazwa kwenye matangi manne, ila hayatoshelezi mahitaji halisi, bali humalizika kwa siku moja.

"Mahitaji ya maji yameongezeka kutokana na joto kali. Tunajitahidi kuhakikisha watoto wanapata maji ya kunywa, lakini changamoto za gharama na miundombinu zinatufanya tushindwe kufikia mahitaji yote," anatamka Mwalimu Mfwangawo.

Anafafanua kuwa mahitaji ya maji kwa siku shuleni ni walau lita 1,500, hivyo kuna uhitaji wa matangi ya nyongeza kufikia kiwango kinachowatosheleza wanafunzi waliopo.

Kuhusu usafi na usalama wa maji hayo, mwalimu huyo anasema "shule yetu inatumia dawa aina ya 'water guard' kutibu maji, kila siku jioni."

### WANAFUNZI WANENA

Mmoja wa wanafunzi, Yerenus Ponela, ambaye ni mwanachama wa Klabu ya Mazingira ya Wakulima Chipukizi iliyopo shuleni, anakiri kukabiliwa na joto kali, inayowafanya wanywe maji mengi, ikilinganishwa na ilivyokuwa awali.

Anasema kwa sasa, ana uwezo wa kunywa zaidi ya lita moja kwa siku akiwa shuleni, ikilinganishwa na awali, alivyotumia kiwango kidogo.

Klabu ya Wakulima Chipukizi, imeanzishwa kupitia mradi wa 'Pamoja Tudumishe Elimu,' unaotekelezwa shuleni Kawe 'A' kupitia ushirikiano wake na asasi binafsi, Shirika la WeWorld,

Ni mradi wa wanafunzi kuhifadhi mazingira, kuwa sehemu ya kuwashirikisha katika vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.



Baadhi ya matangi ya maji yaliyowekwa katika Shule ya Msingi Kawe A kwa ajili ya wanafunzi kunywa. **PICHA ZOTE: GRACE MWAKALINGA**

Ongezeko la joto ardhini, linatajwa kuwa matokeo kubadilika tabianchi, ikiwa na athari kubwa kwa watoto.

Aidha, Ripoti ya Shirika la Kuhudumia Watoto Ulimwenguni (UNICEF) iitwayo 'The State of the World's Children 2024' inataja uhaba wa maji una changamoto kwa mabadiliko ya tabianchi, hata kuwaathari watoto na kundi la vijana balehe.

Ripoti hiyo ya mwaka 2024, inataja athari nyingine ni kuongezeka magonjwa ya kuhara, yanayotokana na mafuriko, kwa sababu ya kujaa mito, mifereji na mabwawa, maji yakisambaa kwenye makazi ya watu.

"Magonjwa haya ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya vifo kwa watoto walio chini ya miaka mitano," inaeleza maudhui ya ripoti hiyo.

### USAFI NA MAZINGIRA

Shule ya Msingi Kawe 'A' ina kisima cha maji chenye ujazo wa lita 5,000 yanayotumika vyooni, kupitia miundombinu iliyojengwa kwa msaada wa mdau, asasi hiyo binafsi. Mfumo wa maji vyooni pia hupokea maji kutoka kwenye kisima hicho, yakiunganishwa na yatokayo DAWASA, hata kuwezesha watoto kunawa watokapo maliwatoni, ikiwa ni hatua ya kuwalinda dhidi ya magonjwa ya kuambukiza.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mfwangawo, shule ina matundu 31 ya vyoo yaliyounganishwa kwenye mfumo wa majitaka. Kati yake, 22 ya wasichana na tisa wavulana.

### MIONGOZO KIMATAIFA

Upatikanaji huduma za majisafi na majitaka, imo katika yanayotajwa kuwa maazimio ya Mkutano wa Watoto na Vijana Balehe 150, uliofanyika Dar es Salaam, Oktoba 2023.

Ni watoto na vijana waliounganа na wenzao, zaidi ya 12,000 kutoa maoni kupitia mpango ulioitwa 'U survey', ulioratibiwa na Umoja wa Mataifa kupitia Ofisi za Tanzania za Shirika la Watoto Duniani (UNICEF).

Ni maoni yaliyokusanywa kati ya Julai na Oktoba mwaka jana, 2023 kutoka watoto na vijana balehe nchini na hatimaye kuwezesha kuandikwa ripoti iliyobeba mtazamo wa jumla wa kundi hilo, inavyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Ripoti hiyo ya utafiti inayoitwa "Children for Climate Action Voices from Tanzania" (Hatua za watoto na mabadiliko ya tabianchi: Sauti kutoka Tanzania), inataja masuala ya kundi hilo linayaona kuwa changamoto katika makuzi na maendeleo yao.

### CHANZO CHA UHABA

Ndani ya changamoto hizo, kuna uhaba wa maji unaosababishwa na ukame katika maeneo, kuliko kawaida na ufyekaji holela wa misitu.

Wanasema ni hali inayowanyima haki zao za msingi, ikiwamo ulinzi katika maeneo ya vijijini wanakofuata huduma husika, wanahatarisha maisha yao.




Katika mapendekezo yao, wanasema: "Watoto na vijana-balehe wanatoa wito kwa serikali na wadau wake wa maendeleo kuchukua hatua za kuwezesha upatikanaji wa maji katika maeneo yanayofikika ili kuwalinda dhidi ya vitendo vya uonevu na unyanyasaji."

Utafiti wa U-Report, unasema asilimia 60 ya watoto na vijana waliohojiwa hawajifunzi vya kutosha changamoto za tabianchi wakiwa shuleni, huku asilimia 80 wanataka mafunzo hayo muhimu kwao, kwa sasa na siku zijazo.

"Tunapendekeza mada za tabianchi katika mafunzo yanayotumia sanaa, kama vile nyimbo za kuelimisha masuala hayo, ili kuongeza ufahamu wa kila siku kuhusu uwajibikaji wa kimazingira," inasomeka sehemu ya ripoti hiyo.

### MIRADI INAYOENDELEA'

Shuleni Kawe 'A', Mwalimu Mfwangawo anataja haja ya kukabiliana na ongezeko la joto kali, wanafuata suluhu kwa njia ya ushirikishwaji wakianza kuwafundisha wanafunzi namna ya kuhifadhi na kutunza mazingira.

Anasema ushirikishwaji huo unafanyika kupitia Mradi wa Pamoja Tudumishe Elimu unaotekelezwa kwa kushirikiana na WeWorld, lengo likiwa ni kuwasaidia watoto kupata elimu ya vitendo ili waweze kukabiliana na changamoto za mazingira wanapokuwa shuleni na hata wakiwa nyumbani.

"Watoto wamefundishwa kulima mboga kama mchicha, nyanya na maboga. Kilimo hicho huchangia siyo tu lishe bora, bali pia huimarisha afya zao kwa kupunguza uwezekano wa kushambuliwa na magonjwa yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kama pumu na saratani ya ngozi," anasema Mwalimu.

Mwanafunzi wa darasa la tano, katika shule hiyo, Mulhat Majid Issa ambaye ni mwanachama wa Klabu ya Mazingira ya Wakulima Chipukizi, anasema walimu wamewafundisha umuhimu wa kutunza mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mulhat anasema, elimu hiyo wanaifanya kwa vitendo wakilima bustani za mboga, matunda na upandaji miti na inawasaidia kutambua umuhimu wake kwa mustakabali wa maisha yao ya baadaye.

### KLABU YA MAZINGIIRA

Pendekezo jingine, linalotokana na kuanzishwa kwa klabu za mazingira katika shule za msingi na sekondari.

"Serikali inapaswa kuanzisha vilabu mbalimbali katika shule za msingi na sekondari na kwenye jamii ili kukuza uhifadhi wa mazingira," anasema binti, aitwaye kwa jina moja Agnes (16) wa mkoani Mbeya.

Katika hilo, mradi wa Pamoja Tudumishe Elimu unaotekelezwa shuleni Kawe 'A' kupitia ushrikiano na Shirika la WeWorld ambako wanafunzi wanafanya kazi za uhifadhi wa mazingira kupitia Klabu ya Wakulima Chipukizi.

Mwalimu Mfwangawo anasema, kupitia programu ya upandaji miti inayofanywa kwa kushirikiana na wanafunzi wanaounda klabu hiyo, miti 60 imeshpandwa kuzunguka maeneo ya shule, ikiwa hatua ya kupunguza ukame na kuhifadhi uoto wa asili.

"Lengo la shule yetu ni kupanda miti 50 zaidi hasa ya matunda, ili kuhakikisha wanafunzi wanapata kivuli na lishe bora, kupitia juhudi hizo, watoto wanajifunza umuhimu wa mazingira na jinsi ya kuyatunza," anasema.

AFYA

### ABAINI AKIWA NA UMRI MIAKA 40...

# Mwanamke aliyehisi hana wazazi halisi, awasaka kimtandao, awapata 'uso kwa uso'

- Hisia zamfunguka 'wazazi' alio nao wameshafariki
- Mama halisi alipohisiwa akakwepa, bado ikashindikana
- Akagundua nyuma ya pazia, ni mtoto wa shangazi yake

**Na Mwandishi Wetu**

Ni simulizi ya aina yake, panaposhuhudiwa utashi na mshangao, mwanamama mwenye umri wa kati kutoka Marekani, Tamona Mosridze, amehisi wazazi wake sio sahihi, pia historia ya maisha yake.

Akiwa na mawazo hayo, akadodosa dalili za ukweli ulioko, pale anawapopigia simu anayemhisi ndiye ana aina ya majibu yanayomfikia.

Dodosa yake ni kumpata mwanamke mama yake halisi. Kwake, mawazo hayo yakaonekana kama ndoto.

Tamona anasimulia: "Kilichomshangaza ni ile hali ya ubaridi na hasira ya yule mwanamke wa upande wa pili wa simu, ananitamkia kwa kelele, hata kufikia kulia... 'sijawahi kupata mtoto na sitaki kuzungumza nami...

"Majibu yake yalinishangaza zaidi kuliko alivyonikasirisha. Nilikuwa tayari kwa lolote, lakini majibu yake yalikuwa zaidi ya vile ambavyo ningeweza kufikiria."

Tamona, mwenye umri wa miaka 40, sasa analitafsiri hilo tukio la Agosti mwaka huu, huenda mhusika hapendi kuhusishwa na hayo maishani mwake.

Lakini Tamona hakukata tamaa kirahisi, akataka kujua jinsi alivyolelewa, baba yake ni nani, siri ambayo mama yake ndiye pekee anaweza kuifafanua.

Wakati ni hatua hiyo kufikiwa, lakini Tamona alianza kumtafuta mama huyo mnamo mwaka wa 2016, pale alipokuwa anasafisha nyumba ya mama yake.

Hapo akashangaa kupata cheti cha kuzaliwa, jina la Tamona likaandikwa kwenye nyaraka hiyo, lakini tarehe yake ya kuzaliwa hakuamini ilikuwa sahihi.

Hiyo ikamfanya ashuku kuwa anaweza kuwa 'mtoto wa kulelewa' na baada ya kufanya utafiti, akaanzisha kikundi cha mtandao wa 'facebook' kisomeka kwa Kiingereza "I'm Looking,"(ninamtafuta) kwa matumaini ya kupata wazazi wake halisi.

Pia, akafichua ulanguzi wa watoto ulioko huko Georgia, Marekani, akitaja inabadilisha maisha ya mamia ya watu.

Kwa miongo kadhaa wazazi walidanganywa, wakidai watoto wao wamekufa wakiwa, kumbe wanauzwa.

Tamona, ambaye kitaaluma ni mwandishi wa habari kupitia mtandao huo akaunganisha mamia ya familia kupitia kazi yake, lakini binafsi hakufichua siri ya maisha yake ya zamani, siri yake akiamini, huenda ametekwa nyara akiwa mtoto.

"Nilikuwa nashughulikia kesi hii kama mwandishi, lakini pia ilikuwa kusudio langu binafsi," anasema.

Hapo akaaanza msako na kupokea ujumbe kupitia ukurasa wake wa 'facebook', ndio pale mmoja anayeishi vijijini vya Georgia, akamfahamisha kumjua mwanamke aliyemficha ujauzito wake na alijifungua huko Tbilisi mnamo Septemba, 1984.

Ni tarehe ya kuzaliwa ambayo mtu, iliyolingana na ile ya Tamona aliyoichapisha kwenye mitandao ya kijamii; mwanaume huyo aliamini kuwa mwanamke huyu ndiyo mama yake Tamona, huku akimpa Tamona hata jina lake halisi.

**WALIOMZAA KAKA NA DADA**

Tamona akaanza mara moja kumtafuta mtandaoni, lakini hakuweza kumpata, hata akaamua kutuma ombi kwenye mtandao wa 'Facebook' kuwauliza kuwapo anayemfahamu.

Mwanamke mmoja akajibu haraka kwamba mwanamke aliyeficha ujauzito wake ni shangazi yake, lakini akamwomba Tamona aondoe chapisho hilo na akakubali kupimwa DNA.

Wakiwa wanasubiri majibu ya DNA, Tamona aliwasiliana na mama yake.

Wiki moja baadaye, matokeo ya DNA yakatoka kwa kuthibitisha Tamona na mwanamke huyo kwenye Facebook walikuwa mabinamu.

Kwa ushahidi huo, Tamona akaamua kumshawishi mama yake kukiri ukweli na kufichua jina la baba yake, ndipo akapatiwa, lilikuwa Gorgon Khoruwa.

"Miezi miwili ya kwanza ilikuwa ya kushangaza," anasema na kuongeza: "Sikuamini haya yote yaliyokuwa yakitokea. Sikuamini kuwa nilikuwa nimewapata."

Baada ya kupokea jina hilo la baba, Tamona akampata haraka kwenye mtandao wa 'facebook' akibaini ni mfuasi wake Tamona kwenye mtandao huo wa kijamii.

Leo hii, kazi ya Tamona katika kuunganisha familia sasa inajulikana sana kote nchini Georgia, akiwa kwenye orodha ya marafiki zake kwa miaka mitatu; awali Gorgon hakujijua kuwa sehemu ya hadithi ya Tamona.

Wakapanga kukutana haraka huko Zugdidi, Magharibi mwa Jimbo la Georgia alikozaliwa, umbali wa kilomita 260 kutoka nyumbani kwa Tamona huko Tbilisi.

Sasa Tamona, anakumbuka siku za nyuma hilo lilimshtusha sana, leo hii lina mvuto.

Kimsingi, mama huyo akaanza kumsaka na mzee huyo mwenye umri wa miaka 72 na alipofika kukutana naye, akisimulia walikumbatiana kwa furaha, kisha wakasimama kwa muda kutazamana kwa tabasamu.

Tamona anasimulia: "Ilikuwa ajabu, aliponitazama, alijua mimi ni binti yake. Tulikuwa na hisia mseto sana."

Lakini bado moyoni, Tamona akawa na maswali mengi na hakujua pa kuanzia, akidokeza: "tuliketi tu, tukatazamana na kujaribu kutafuta pa kuanzia."

**AFANANA NA UKOO WOTE**

Walipokuwa wakizungumza, anasema akagundua kwamba walikuwa na mengi ya kufanana.

Gorgan, wakati mmoja alikuwa mcheza dansi maarufu huko Georgia, pia alifurahi kwamba Tamona (wajukuu zake) walipenda kucheza hivyo.

"Binti zangu wote wawili wanapenda kucheza dansi, pia mke wangu," anasimulia na kucheka.

Gorgon akaialika familia yake yote nyumbani kuonana na Tamona, hata akawatambulisha kwa kundi kubwa la jamaa zake; akikutana na kaka na dada zake, wajombae, wanawe na wakwe zake.

Kila mtu katika familia akakubali Tamona anafanana sana na baba yake, mwenyewe anayefananishwa, akiunga mkono kwa hoja "kati ya watoto wake wote, nilifanana zaidi na baba yangu."

Hapo wakatumia jioni hiyo, kukumbuka mambo yaliyopita, kula chakula chao kimila, wakaimba nyimbo za kikwao - Georgia na kucheza huku wakipiga kinanda maalum.



Tamona Mosridze, akiwa na baba yake halisi baaada ya kumpata. **PICHA: MTANDAO**

**SWALI TATA LILILOBAKI**

Swali moja bado lilibaki akilini mwake Tamona, kama je, alitekwa nyara kutoka kwa mama yake wakati wa kuzaliwa, au aliuzwa?

Kwa kuwa baba na mama yake walezi wamekufa, akashindwa kupata majibu na hatimaye, mwezi Oktoba uliyopita, Tamona akapata fursa ya kumuuliza uhalisia wa mama yake ni nani.

Kituo cha televisheni cha Poland kilikuwa kikitengeneza filamu kuhusu Tamona na kumpeleka kukutana na mama yake. Mama yake akakubali kuongea naye faragha.

**MZIZI WA KUZALIWA KWAKE**

Tofauti na watu wengi ambao Tamona akawasaidia kuungana na familia zao, akagundua kwamba hakuwa ametekwa nyara akiwa mtoto.

Ni kwamba mama yake alikuwa amemwacha na kuficha siri hiyo kwa miaka 40 na wazazi wake hawakuwa na uhusiano, bali walikuwa pamoja kwa muda mfupi tu.

Mama yake akaona aibu sana wakati huo na kuamua kuficha ujauzito wake mnamo Septemba 1984, aliposafiri kwenda eneo la Tibilisi, kwa kisingizio cha upasuaji.

Ukweli ni kwamba, binti yake alibaki huko hadi mchakato wa kuasili wa Tamona ulipokamilika.

"Nilipogundua kuwa nimechukuliwa na mtu mwingine na nilikuwa nimekaa kwa siku kumi tu na mama yangu, nilihisi uchungu sana," Tamona anasema kwa huzuni, akinena "ninajaribu kujizuia kufikiria hilo."

Sasa, anaamini si haki kwa kinamana na baba, kuwa na nyendo kama hizo za watoto wao kupotoshwa.

Sasa anafafanua, uhalisia penye udanganyifu wa aina hiyo, ni ngumu kuwapo atakayeamini uhalisia wa upotoshaji wa kinamama kwa aina hiyo.

Baadaye, mama yake akamwomba aondoke nyumbani na hawakuzungumza tena baada ya hapo.

Leo hii anasema: "Je, niko tayari kupitia hatua hizi zote tena? Kwa kweli, ndivyo nilivyofanya, nilijifunza mengi kuhusu familia yangu mpya."

• ***Kwa mujibu wa BBC***



# Ridhiwani apinga wenye ulemavu kubaguliwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete amepinga ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu sehemu za kazi ili kuwe na usawa kwa watu wote.

Ridhiwani alitoa kauli hiyo jana jijini Dodoma wakati akifunga mafunzo ya usalama, afya, haki na wajibu kwa watu wenye ulemavu yaliyoandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa kushirikiana na Mahakama Kuu-Divisheni ya Kazi.

"Mkataba namba 159 wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) unahimiza usawa katika masuala ya kazi kwa watu wote bila kujali wana ulemavu au la kwa kuwa takwimu zinaonesha asilimia 15 ya watu wote duniani ni wenye ulemavu na moja ya changamoto za kundi hili ni kufanyishwa kazi zisisokuwa na staha na kubaguliwa," alisema.

Alisema kutokana na Tanzania kuwa mwanachama wa ILO, itaendelea kuhimiza utendaji wa kazi zenye staha na kupinga vikali ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu.

Alisema mafunzo yanayotolewa na OSHA ni utekelezaji wa wajibu wa serikali wa kulinda nguvukazi yake kupitia usimamizi wa Sheria namba tano ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 na kuitaka OSHA kuendelea kutekeleza wajibu huo ipasavyo kwa makundi mbalimbali katika jamii.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alieleza sababu za wakala huo kushirikiana na Mahakama kuwa ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali ya mifumo yake kusomana.

Awali, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu Tanzania, Dk. Mustapher Siyani aliipongeza OSHA na Mahakama Kuu-Divisheni ya Kazi kwakuandaa mafunzo hayo kwa watumishi wa serikali.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu-Divisheni ya Kazi, Dk. Yose Mlyambina, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha walengwa kushiriki katika mapambano dhidi ya magonjwa, ajali, vifo na madhira mengine yanayotokea mahali pa kazi na kutambua haki na wajibu wao katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

# Waziri aitwisha zigo NARCO

**Na Thobias Mwanakatwe,**
DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Ashatu Kijaji ameagiza Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mifugo, malisho na upatikanaji wa nyama nchini ili kukuza uchumi wa sekta ya mifugo.

Kijaji, alitoa maagizo hayo juzi baada ya kutembelea Ranchi ya Kongwa iliyopo Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma na kuahidi kurudi Januari 5, mwakani kufuatilia utekelezaji wa maagizo hayo.

"NARCO mnajukumu la kuzalisha mbegu bora za aina mbalimbali, Watanzania wanahitaji mifugo inayouzika kwa urahisi ndani ya nchi na kimataifa, tunataka kila mfugaji akiuza ng'ombe apate Sh. milioni nane, nawataka mzalishe mbegu bora kwa ajili ya wafugaji wetu," alisema.

Kuhusu uzalishaji wa mbegu za malisho, Kijaji alimuagiza Mkurugenzi wa Uzalishaji na Maendeleo ya Masoko, Stephen Michael kushirikiana na NARCO ku-

**Kijaji, alitoa maagizo hayo juzi baada ya kutembelea Ranchi ya Kongwa iliyopo Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma na kuahidi kurudi Januari 5, mwakani kufuatilia utekelezaji wa maagizo hayo.**

kamilisha malipo ya mkandarasi wa mradi wa visima sita wenye thamani ya Sh. milioni 700 ili vianze kuzalishia malisho.

" Tumetembelea mradi wa visima hapa NARCO ni mkubwa serikali imetoa Sh.milioni 700, lakini umekwama kwa sababu ya madai ya mkandarasi, sasa nataka nitakaporudi hapa Januari 5, 2025 visima na mabirika haya ya kunyweshea ng'ombe nikute yameanza kutumika," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya NARCO, Aziz Mrima, alisema bodi hiyo inajukumu la kuifanya kampuni hiyo izalishe mbegu bora za mifugo zitakazoweza kushindana na wafugaji wengine barani Afrika na kuahidi kutekeleza maagizo ya WaziriKijaji.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Maendeleo ya Masoko, Stephen Michael, alisema idara yake itaendelea kufuatilia mradi huo ili kuhakikisha unakamilka kwa wakati.

Michael, alisema hadi sasa Sh. Bilioni 3.2 zimepatikana kwa ajili ya malipo ya mradi huo.




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Ashatu Kijaji (mwenye fimbo), akikagua ng'ombe bora wanaopatikana kwenye Ranchi ya Taifa (NARCO LTD) iliyopo Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma baada ya kuitembelea jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Profesa akerwa wanafunzi kubebeshwa mafaili ofisini

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAHITIMU wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) wametakiwa kuhakikisha wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo kwenye ofisi zao wanapata uzoefu badala ya kuwatuma kukoroga chai na kubeba mafaili.

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa IFM, Profesa Josephat Lotto wakati wa hafla ya chakula cha usiku ya wanafunzi waliosoma zamani katika chuo hicho iliyofanyika jijini hapa.

Profesa Lotto, alisema wanafunzi wa vyuo mbalimbali nchini wanapokwenda katika ofisi kwa mafunzo kwa vitendo, wengi wanaishia kutumwa kubeba mafaili na kukoroga chai, hivyo kushindwa kupata kile walichokusudiwa na kurudi chuoni wakiwa hawana kitu kichwani.

"Hili linasikitisha sana kwa sababu wanafunzi wanarudi chuoni wakiwa hawajapata kitu,naomba nyie kama ALUMNI (wanafunzi wa zamani wa IFM) mliopo katika ofisi mbalimbali kuwasaidia wanafunzi hao ili wakihitimu waweze kuajirika au kujiajiri wao wenyewe,"alisema.

Alisema kama wadau,wakiamua kuwasimamia wanafunzi hao ipasavyo, watapata uzoefu wa kutosha na kufanya vizuri kwa vitendo watakapoajiriwa na kujiajiri.

Alitoa rai kwa ALUMNI kuwa sehemu ya mkakati wa chuo hicho wa kuanzisha sehemu ambayo itahusisha waajiriwa waliomaliza IFM kutoka taasisi tofauti pamoja na wanafunzi ili kuwasaidia kufanya majaribio na kupata kile walichokusudia.

"Wanafunzi waliofikia muda wakwenda kufanya mafunzo kwa vitendo wataingia kwenye platform hiyo pamoja na waajiri,hii itakuwa imesaidia kufanya majaribio kwa vitendo kupitia platform,"alisema Profesa Lotto.

Alisema katika kuisadia serikali kuzidi kuinua kiwango cha elimu nchini, alisema IFM kimebuni mkakati wa kupeleka madaftari yenye nembo ya chuo hicho katika shule mbalimbali nchini kukitambulisha kwao baada ya kuhitimu masomo yao.

Profesa Lotto, alisema lengo ni kuwashawishi wanafunzi kupenda hisabati ambalo katika kozi nyingi zinazotolewa chuoni hapo ni somo hilo ni la lazima.

Alisema wameanza na shule 184 katika wilaya 40 za mikoa sita na kwamba wanahitaji Sh. milion 52.8 ili kufanikisha mkakati huo.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, ambaye ni miongoni mwa ALUMNI, Abdulmajid Nsekela alimpongeza mkuu huyo wa wa chuo hicho na timu yake kwa kubuni mikakati ya kuboresha elimu nchini.

Nsekela, alisema mkakati wa kushawishi wanafunzi kupenda hisabati na kukitangaza chuo hicho kwa wanafunzi ni mzurikwa kuwa utaongeza wigo wa wanafunzi kujiunga na kusoma kozi mbalimbali.

Alisema wao kama ALUMNI, watashirikiana na IFM kuhakikisha inazidi kutanua wigo wa kutoa elimu ndani na nje ya nchi ili kuzalisha wataalamu wengi wa fedha.

Kuhusu Sh milioni 52.8 zinazohitajika kwa mkakati wa kupeleka madaftari hayo shuleni kushawishi wanafunzi kupenda kusoma hisabati na kuifahamu IFM,Nsekela aliendesha harambee katika hafla hiyo.

Katika harambee hiyo, ahadi ilikuwa ni sh milioni 36 na fedha tasilimu sh milioni nane..





# Wataalamu TMA, miamba sasa kuchunguza radi Ludewa

## ●Ni kutokana na kuua watu na mifugo mara kwa mara

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WATAALAMU wa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) kwa kushirikiana na wa miamba wanatarajia kufanya tafiti na kudhibiti radi kuendelea kusababisha vifo vya watu na wanyama wilayani hapa Mkoa wa Njombe.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Olivanus Thomas, katika Kijiji cha Kiwe Kata ya Mawengi wakati wa maziko ya watu watatu waliokufa kwa kupigwa na radi Sixbeth Haule (58), Emilian Mlelwa (55) na Lufina Ngailo (52).

Watu hao, walikumbwa na mkasa huo Desemba 15, mwaka huu majira ya saa 11 jioni katika Kijiji cha Kiwe, wakati watu hao wakiwa wamesimama nyumbani kwa Ngailo.

Thomas, alisema wiki mbili zilizopita watu wengine wanne walikufa kwa kupigwa radi, watatu wakiwa wa familia moja.

"Serikali tumeanza kufanya mawasiliano na Mamlaka ya Hali ya Hewa pamoja na wataalamu wa miamba ili waweze kuja kufanya tafiti na tujue namna gani tunaweza kudhibiti radi hii," alisema.

Alisema radi ni suala la hali ya hewa na kwa upande wa ardhi inafuata maeneo yenye miamba.

"Mtaalamu mmoja alinieleza watu wengi wanasema mvua ilikuwa kidogo ndio radi ikatokea, kwanini inapofika mwezi wa pili au watatu mvua zinakuwa nyingi hakuna radi. Radi wakati wote ni umeme ambao unatokana na mawingu," alisema.

Aliwataka wakazi wa wilaya hiyo kuachana na imani potofu kwa kuhusisha vifo vinavyotokana na radi na mambo mengine badala yake wanapaswa kutambua kuwa ni mipango ya Mungu.

Akitoa taarifa kuhusu vifo vya watu hao, pamoja na mambo mengine, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, alitoa tahadhari kwa wananchi kuacha kukaa kwenye maeneo ambayo yana mvutano na radi ili kuepuka vifo vya aina hiyo.

Banga, alisema wataendelea kutoa elimu kupitia wakaguzi wa kata kuhimiza wananchi kuweka vikinga radi kwenye nyumba zao.



Katibu wa Sekreterieti ya Kamati Kuu ya Chadema Julias Mwita akimkabidhi fomu Dorcas Francis kwa ajili ya kuwania nafasi ya ujumbe wa kamati kuu, katika ofisi za makao makuu ya chama hicho, Mikocheni Dra es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara waamriwa kurejea sokoni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BAADHI ya wafanyabiashara wa Halmashauri ya Mji wa Njombe wametakiwa kuondoka kwa hiyari kwenye maeneo yasiyo rasmi ili kukwepa mkono wa sheria.

Amri hiyo ilitolewa juzi na Mtendaji wa Kata ya Njombe Mjini, Enocy Lupimo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Njombe Kuruthum Sadick wakati wa kampeni ya kufanya usafi katika Mtaa wa Buguruni.

Lupimo, alisema halmashauri hiyo imeagiza wafanyabiashara waliotoa bidhaa sokoni na kupeleka barabarani kuondoa kabla hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

"Lazima tujizatiti katika suala la usafi na ninapeleka salamu stendi ya zamani, mkurugenzi ametoa vizimba soko kuu watu wanatoka wanaenda kupanga bidhaa stendi, kama una shangazi anauza pale vitumbua waambieni watoke kwa hiyari," alisema.

Akizungumzia kuhusu usafi, alisema kampeni hiyo ni mwendelezo ili kutunza mazingira katika mitaa yote tisa ya kata hiyo na kudhibiti kuibuka kwa magonjwa ya milipuko.

Mratibu wa Chanjo Halmashauri hiyo, kwa niaba ya Ofisa Afya, Simon Ngassa, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kufanya usafi ili kujikinga na maradhi yanayotokana na uchafu.

"Tuchukue tahadhari zote za usafi lakini pia watoto wapate chakula cha moto na wale wafanyabiashara yaani mama lishe wanaotuhudumia hakikisheni kwenye mgahawa mna maji safi ya kunawa na sabuni ya maji sio kipande, pia muwaeleze wale wanaofanya biashara barabarani warudi sokoni," alisema Ngassa.

Polisi Kata wa Njombe Mjini, Frolida Kietta aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka kwa kuongeza ulinzi kwa watoto ili kuepuka ukatili wa kijinsia.

# TASAF yaondoa chanjo kwenye turubai

**Na Faustine Feliciane**

UJENZI wa jengo la kutolea huduma ya mama na mtoto uliofanywa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Kituo cha Afya cha Makole jijini Dodoma umeondoa adha ya kupata chanjo kwenye turubai.

Kabla ya ujenzi wa jengo hilo, wakazi wa Kata ya Makole na maeneo ya jirani ya Swaswa na Ipagala walikuwa wakipatiwa huduma ikiwamo chanjo kwenye mazingira yasiyo rafiki.

Akizungumza kuhusu ujenzi wa jengo hilo uliofanywa na TASAF , Mtendaji wa Kata hiyo, Suzan Yohana, alisema wakazi hao walikuwa wanapata adha kwa kunyeshewa mvua wakati wa masika na vumbi kiangazi na kukosa hewa safi kwa kuwa eneo lilikuwa limefungwa turubai kwa ufinyu.

"Imekuwa faida kwetu na tunawashukuru TASAF kwa kujenga jengo hili ambalo sasa limesaidia huduma kutolewa katika mazingira bora zaidi, TASAF wamekuwa wadau wazuri sana katika kuboresha huduma hizi za mama na mtoto," alisema Yohana.

Kaimu Muuguzi Mfawidhi wa Kituo hicho, Joyce Kimario, alisema idadi ya watu waliokuwa wakifika kupata huduma katika kituo hicho ilikuwa ndogo ikilinganishwa na sasa baada ya mfuko huo kuwajengea jengo hilo.

Mwanakamati anayeshughulikia mpango wa walengwa wa TASAF ngazi ya mtaa, Neema Tandi alisema: "Wakati kukiwa na turubai kuna muda huduma zilikuwa zinasimama kutokana na upepo na mvua kusababisha kuanguka.

**Kabla ya ujenzi wa jengo hilo, wakazi wa Kata ya Makole na maeneo ya jirani ya Swaswa na Ipagala walikuwa wakipatiwa huduma ikiwamo chanjo kwenye mazingira yasiyo rafiki.**



## Watalii wazidi kumiminika Unguja, Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDADI ya wageni waliyoingia visiwani hapa mwezi uliopita imeongezeka hadi kufikia 67,049 kwa mwaka huu.

Takwimu hizo zilitolewa jana na Ofisa Tafiti na Takwimu wa Kamisheni ya Utalii, Hassan Ameir Vuai wakati akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa.

Vuai, alisema idadi hiyo ni kubwa wageni hao walioingia visiwani hapa Novemba mwaka huu ni kubwa ikilinganishwa na 57,296 walioingia mwezi huo mwaka jana.

Alisema idadi hiyo inaonesha ongezeko la asilimia 17.0 ikilinganishwa na asilimia 4.0 ya mwaka jana.

Vuai, alisema kati ya wageni hao, 48,919 waliingia Zanzibar kutoka Bara la Ulaya sawa na asilimia 73.0 ikifuatiwa na Afrika 9,750 sawa na asilimia 14.5 .

Alisema Asia 4,096 sawa na asilimia 6.1 na Iceania lilikuwa la mwisho kwa kuwa na 504 sawa na asilimia 0.8.

Vuai, alisem nchi ya italia iliongoza kwa kuleta wageni 7,519, ikifuatiwa na 6,299 na Polishi 5,558.

Alisema Ujerumani ilishika nafasi ya nne kwa kuingiza wageni 5,385, Uingereza 3,206

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, Mipango na Utawala Kamisheni ya Utalii, Aviw Issa Makame, alisema kuongezeka kwa idadi ya watalii Zanzibar kunatokana na juhudi za serikali kutangaza sekta hiyo kwenye mikutano na makongamano.

**Alisema idadi hiyo inaonesha ongezeko la asilimia 17.0 ikilinganishwa na asilimia 4.0 ya mwaka jana.**

# Mwinyi asifia ukaguzi wa CAG kuimarisha huduma za jamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema ukaguzi wa rasilimali za umma unaofanywa na Ofisi ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kila mwaka, umechochea kuimarisha utoaji huduma za jamii visiwani hapa.

Dk, Mwinyi aliyasema hayo jana katika kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Ukaguzi yaliyofanyika mjini hapa yenye kauli mbiu isemayo"Kuimarika kwa ukaguzi wa rasilimali za umma kunaongeza ufanisi na kuleta tija nchini.".

Alisema ukaguzi huo wa rasilimali fedha na nyingine umesaidia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, bandari, viwanja vya ndege, viwanja vya michezo na masoko.

Alisema mafanikio hayo yamekuja baada ya Serikali kupokea na kuzifanyia kazi hoja, ushauri na mapendekezo yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kupitia ripoti zake za kila mwaka.

"Napenda kuchukua fursa hii kupongeza jitihada zinazochukuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuimarisha utawala bora nchini," alisema.

Alisema kuimarisha utawala bora ni jambo la msingi kuleta maendeleo nchini, hivyo ni lazima kila mmoja kuongeza juhudi, uzalendo na uadilifu kuitumikia nchi.

Mwinyi, alisema Serikali itaendelea kuijengea mazingira mazuri Ofisi ya CAG ili kutekeleza kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni, na taratibu kitaifa na kimataifa na kwenda sambamba na mabadiliko ya mara kwa mara ya ukaguzi duniani.

"Wajibu wa kuimarisha Utawala Bora katika matumizi ya rasilimali za umma si wa Serikali na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pekee bali ni letu sote," alisema.

CAG Zanzibar, Dk. Othman Abbasi Ali, alisema katika maadhimisho hayo, wataalamu wao wamebadilishana uzoefu na kujifunza mbinu za kukabiliana na rushwa na uhujumu uchumi, kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Ali, alisema utaratibu wa kusomwa kwa taarifa ya CAG hadharani na kujadiliwa kwa kina na uwazi kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar umeleta mafanikio makubwa kujenga uelewa kwa wananchi juu ya matumizi ya fedha za umma.



Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, akibadilishana mawazo na Mkuu wa Kikosi cha KVZ, Meja Said Ali Shamuhuna katika hafla ya kuwapongeza KVZ Queens iliyofanyika Mtoni Wilaya ya Magharibi A, Zanzibar jana, baada ya kupata ushindi katika Kombe la Muungano lililofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zanzibar, China kuendeleza zao la nazi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kushirikiana na wadau kuendeleza zao la nazi ili kuongeza kipato kwa jamii na manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Waziri wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis aliyasema hayo wakati akifunga mafunzo ya kuendeleza, kudhibiti maradhi ya wadudu waharibifu katika zao hilo yaliyotolewa na wataalamu kutoka nchini China.

Shamte, alisema hali ya ustawi wa zao hilo inatisha hivyo kuna haja ya kuweka kipaumbele cha kuimarisha na kuendeleza kwa kuwa ni muhimu kwa biashara na kuongeza pato la Zanzibar.

Alisema zao hilo lina umuhimu mkubwa katika kupendezesha mandhari ya nchi na kufanya kiungo muhimu katika miundombinu ya utalii ambao upo hatarini kutoweka.

Alisema mbali na changamoto hizo, zao hilo linashambuliwa na maradhi na wadudu na kuwa changamoto kwa ustawi.

Alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa lengo la kuendeleza program ya Minazi nchini kwa Wizara ya Kilimo kuweka malengo ya kuotesha miche 300,000 kwa mwaka 2024/2025 na kuisambaza bure kwa wananchi.

Mwakilishi wa Balozi wa China nchini. Wang Yu, alisema Serikali yao ni rafiki wa kudumu na Serikali ya Zanzibar na ndiyo maana wakaona ipo haja ya kushirikiana kuandaa mafunzo hayo kwa wataalamu wa kilimo ili wawe mabalozi wazuri kwa wakulima.

Alisema kuwa China imepitia hatua kubwa katika sekta ya kilimo hivyo matumaini yake baada ya mafunzo hayo wataalamu hao watayafanyia kazi ili Zanzibar kuendelea kupiga hatua katika sekta ya kilimo.

Mratibu wa Mafunzo hayo kutoka Wizara ya Kilimo Zanzibar, Masoud Salum Abdi alisema mafunzo hayo ni mara ya pili kufanyika visiwani hapa kwa lengo changamoto zinazolikabili

# Ajali ilivyokatisha uhai watu 15, kujeruhi saba

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

WATU 15 wamefariki dunia na wengine saba kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha basi dogo la abiria aina ya coaster kugongana na lori katika eneo la Mikese, mkoani Morogoro.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Daniel Nkungu akithibitisha kupokea majeruhi na miili ya watu waliofariki dunia.

Alisema majeruhi saba wamelazwa hospitalini wakiendelea kupatiwa matibabu.

"Majeruhi mmoja alipoteza maisha tulikuwa tukimpeleka Theatre (jengo la upasuaji). Alipata tatizo la mguu pamoja na tumbo, tukiwa tunampeleka theatre, moyo uliacha kufanya kazi na tulijitahidi kadri ya uwezo wetu kumwokoa lakini ikashindikana," alisema Dk. Nkungu.

Alisema kuwa awali walipokea majeruhi wanane na miili 14 na kati ya majeruhi hao, wawili hali zao zilikuwa haziridhishi.

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, CP Awadhi Juma Haji alitaja chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa lori lenye namba za usajili T 715 DZX lililokuwa linatoka Dar es Salaam kwenda Morogoro kutaka kuyapita magari yaliyokuwa mbele yake bila kuchukua tahadhari.

Hivyo, aliwataka madereva kuzingatia sheria na taratibu za usalama barabarani ili kuepusha ajali zinazosababisha upotevu wa rasilimali watu na mali.

Mmoja wa majeruhi, Ally Hengo, ambaye ni Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Pwani na mwandishi wa zamani wa ITV na Radio One, alisema ajali hiyo imetokea wakati wanatokea Morogoro kwenda Dar es Salaam.

"Mbele yetu kulikuwa na foleni ya malori yakitokea Dar es Salaam. Sasa lori moja likatanua (likahama njia) na kukutana na sisi uso kwa uso. Mimi nilikuwa nimekaa siti ya mbele pembeni ya dereva, kama Mungu tu, ajali ilivyotokea nikatupwa nyuma, lile lori likatupiga uso kwa uso, sijui kama yule dereva atakuwa hai," alisema Hengo.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima alifika katika eneo la tukio. Alitoa wito kwa wananchi kufika hospitalini Morogoro kutambua miili ya watu waliofariki dunia katika ajali hiyo.

Alisema: "Japo miili mingine ni ngumu kutambuliwa kirahisi kwa sababu imesagika sana, na hii ajali imechangiwa na uzembe wa madereva. Ni muhimu sana madereva wakachukua tahadhari wawapo barabarani kuepuka ajali zinazoweza kuzuilika," alisema.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) pia ilitoa salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, waathirika wa ajali, ndugu, jamaa na marafiki kufuatia ajali hiyo.

Taarifa kwa umma iliyotolewa na mamlaka hiyo ilieleza kuwa Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi imepokea kwa masikitiko taarifa ya ajali hiyo na kuwaombea majeruhi uponyaji wa haraka na kuahidi itaendelea kuchukua hatua za kiudhibiti ili kuepusha ajali.



Baadhi ya wakazi wa eneo la Mikese, mkoani Morogoro, wakiangalia lori lililogongana na basi dogo la abiria aina ya Toyota Coaster katika barabara kuu ya Morogoro- Dar es Salaam na kusababisha watu 15 kupoteza maisha, saba kujeruhiwa na kulazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro jana.. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Tendwa kuzikwa kesho Dar

**Na Halfani Chusi**

MWILI wa aliyekuwa Msajili wa Vyama vya Siasa Mstaafu, John Tendwa, unatarajiwa kuzikwa kesho katika makaburi ya Ununio kwa Kondo, Dar es Salaam.

Tendwa alifariki dunia usiku wa kuamkia juzi wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Kwa mujibu wa ratiba ya msiba huo iliyotolewa na familia jana, leo mwili wa Tendwa utaagwa katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam kuanzia saa 3:00 asubuhi mpaka saa 8:00 mchana.

Ratiba hiyo ilifafanua zaidi kwamba baada ya tukio hilo, mwili utarejeshwa nyumbani kwake, Kibamba, Dar es Salaam kwa ajili ya taratibu za maziko.

Tendwa alitumikia nafasi hiyo kwa miaka 13 kuanzia mwaka 2001 hadi 2013 akipokea kijiti kutoka kwa George Liundi kisha kumwachia Jaji Francis Mutungi ambaye anaongoza mpaka sasa ofisi hiyo.

Mbali na kuwa mpenda haki, Tendwa pia atakumbukwa kwa kauli yake aliyowahi kuitoa enzi za uhai wake kwamba vyama vya siasa vitakavyobainika kusababisha mauaji, vitafutiwa usajili kutokana na kukiuka sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji shughuli za siasa nchini.

**MUTUNGI AMLILIA**

Akizungumza kwa njia ya simu, jana Jaji Mutungi alisema amepokea msiba huo kwa majonzi makubwa na kwamba (Tendwa) alikuwa mshauri wake mkuu anapokwama.

Jaji Mutungi alisema: "Tendwa ni kaka yangu, kwa kuwa ndiye ameniachia kijiti cha kazi ninayoifanya kwa sasa. Siwezi kuzungumza mengi sana lakini alikuwa mtu muhimu kwangu.

"Bahati mbaya, nilikaa naye kwa muda mfupi kwa sababu wakati ninaingia yeye alikuwa amestaafu. Hata hivyo, alikuwa msaada mkubwa pale nilipokuwa anahitaji ushauri wake."

## Vijana wafundwa kufanya kazi kwa bidii

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MJUMBE wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Iringa, Dickson Mwipopo, ametaka Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Wilaya ya Iringa Mjini kufanya kazi kwa bidii, ikiwamo kujikita kwenye kilimo, ili kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Akizungumza jana katika kongamano la kuwashukuru vijana wa CCM wa wilaya hiyo kwa kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Mwipopo aliwataka vijana kuacha kutegemea misaada, badala yake wajitegemee kwa kufanya kazi kwa juhudi.

Mwipopo alisema Rais Samia Suluhu Hassan amewekeza zaidi ya Sh. bilioni 56 katika ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ili kuboresha sekta ya kilimo na kuwawezesha vijana kujikita katika kilimo biashara.

Alisema mradi huo unapaswa kutumiwa na wakazi wa Iringa badala ya kusubiri watu kutoka mikoa mingine kama Mbeya au Morogoro kutumia fursa hizo.

"Vijana tuache kusubiri kupewa. Rais Samia ametuletea skimu ya kilimo. Twendeni tukafanye kazi kwa bidii. Iringa tuna sifa ya kufanya kazi, tusikubali kurudi nyuma," alisema.

Aidha, aliwataka vijana kuchangamkia mafunzo ya ujuzi mbalimbali ili waweze kujiajiri na kuwa na maisha endelevu badala ya kulalamikia ukosefu wa ajira.

Mwenyekiti wa CCM (UVCCM) Wilya ya Iringa Mjini, Isack Kikoti, alisema vijana walijitokeza kwa wingi na kushiriki kikamilifu katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema CCM ilishinda mitaa yote 192 ya Iringa Mjini na kuonyesha nguvu ya ushirikiano wa vijana.

"Tumemaliza salama uchaguzi wa serikali za mitaa lakini hii ni ishara ya maandalizi yetu kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Tutahakikisha tunazalisha ushindi mkubwa kwa Rais, wabunge na madiwani," alisema.

Kikoti pia alitoa wito kwa vijana kuanza maandalizi ya uchaguzi kwa kuwahamasisha wananchi kujitokeza kuhakiki na kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura.

Kikoti alikiri kuwa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) bado haujawa na miradi ya kiuchumi inayomilikiwa na vijana. Alisema kuwa hali hiyo imewafanya vijana kuwa ombaomba, jambo ambalo alisema linahitaji kutatuliwa.

Hata hivyo aliomba msaada wa kukamilishwa kwa ujenzi wa nyumba ya katibu wa UVCCM ambayo ilisimama kutokana na changamoto za kiuchumi.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Iringa, Tumaini Msowoya, aliwahimiza vijana waliomaliza vyuo vikuu kujiajiri badala ya kutegemea ajira. Alisisitiza kuwa nidhamu ni msingi wa mafanikio katika maisha, kazi na biashara.

"Vijana wenzangu, nidhamu ndio msingi wa mafanikio. Bila nidhamu, huwezi kufanya kazi au biashara kwa ufanisi. Hakikisha unajenga tabia ya nidhamu katika kila hatua ya maisha yako," alisema.

Alitaka vijana kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa kwa kufanya kazi kwa bidii, kujiajiri na kudumisha nidhamu na mshikamano kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

# Russia yamkamata jasusi wa Ukraine kwa mauaji

**MOSCOW, Russia**

IDARA ya usalama ya Russia, imemkamata mwanamume mwenye umri wa miaka 29 kutoka Uzbekistan, akihusishwa na mauaji jenerali wa kijeshi, Igor Kirillov, na msaidizi wake.

Luteni Jenerali, Igor Kirillov, ambaye ni mkuu wa Kikosi cha Ulinzi wa Nyuklia, Biolojia, Kemikali, alilipuliwa na bomu lilofichwa kwenye pikipiki ya umeme iliyowekwa nje ya nyumba yake.

Mlipuaji ambaye alikuwa mbali, alilituhusu bomu hilo kulipuka wakati Jenerali Kirillov na msaidizi wake wakitoka nje ya makazi yake. Idara ya usalama ya Russia ilisema mshukiwa huyo alisajiliwa na idara ya ujasusi wa Ukraine.

Chanzo cha habari cha Ukraine kiliiambia BBC kuwa mauaji hayo yalipangwa na idara ya usalama ya Ukraine.

Chanzo cha usalama cha Ukraine kilisema Kirillov,ambaye alikuwa mkuu wa silaha za kemikali wa Russia alilengwa kimakusudi kwa sababu alitekeleza uhalifu wa kivita.

Jumatatu, siku moja kabla ya mauaji hayo, Ukraine ilimshtaki Kirillov, 54, bila kuwepo mahakamani, ikisema „alihusika na matumizi makubwa ya silaha za kemikali zilizopigwa marufuku".

Kitengo cha mahusiano ya umma cha Shirika la Ujasusi la Urusi kilisema Jumatano kwamba kijana huyo anashukiwa kufanya shambulio hilo la kigaidi.

Taarifa ilisema wakati wa"mahojiano kijana huyo alieleza kwamba aliajiriwa na kitengo maalum cha Ukraine.

Hata hivyo, mauaji ya Luteni Jenerali Igor Kirillov, imeelezwa inaongeza hofu ya usalama dhidi ya raia wa Russia.

"Ni jambo moja kufahamu juu ya hili katika vyombo vya habari, utahisi liko mbali, lakini linapotokea karibu na wewe, hilo ni suala tofauti kabisa na la kutisha," alisema Liza aliponukuliwa na BBC.

Liza anaishi katika jengo moja ambalo lilitokea mlipuko huo.

Aliongeza "wasiwasi wangu umeongezeka kupita kiasi. Kila sauti unayosikia inakushtua, unajiuliza kama ni ndege isiyo na rubani au kitu kimetokea kwenye eneo la ujenzi,"

Mtazamo wa vita vya Russia na Ukraine kama kitu kilicho mbali zaidi, umeanza kubadilika kwa idadi kubwa ya watu.

Kuna dalili kidogo sana kwamba Russia itabadili mwelekeo wake wa vita, badala yake kuna uwezekano kazi ya mapigano yakazidi mara dufu.

Rais wa zamani wa Urusi Dmitry Medvedev, alisema wachunguzi lazima wawapate wauaji waliotekeleza ndani ya Russia.

Rais Vladimir Putin, bado hajazungumzia hadharani mauaji hayo ya jenerali na msaidizi wake.

Hata hivyo, msemaji wa Ikulu ya Kremlin, mara kwa mara amesema endapo Russia itakabiliwa na vitisho vya usalama, wakati wowote ule itajibu vikali.

**BBC**



Kiongozi wa kundi la HTS linaloongoza Syria, Abu Muhammad al-Joulani (kulia) akizungumza na mjumbe maalum wa Umoja wa Mataifa nchini Syria, Geir Pederson, jana. **PICHA: ALLIANCE**

# Netanyahu asisitiza jeshi kukalia mlima Hermon

**TEL AVIV, Israel**

WAZIRI Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, amesema wanajeshi wake wataendelea kubaki katika eneo la kimkakati la Mlima Hermon kwenye mpaka wa Syria hadi mpango mwingine utakapofikiwa kuhakikisha usalama wa Israel.

Netanyahu alilitembelea eneo hilo na kufanya mazungumzo na maofisa wa usalama pamoja na makamanda wa jeshi.

„Niko hapa kwenye kilele cha Mlima Hermon pamoja na Waziri wa Ulinzi, Mkuu wa Majeshi, Kanali wa Kamandi ya Kaskazini, Mkuu wa Shin Bet, na makamanda wakuu. Tuko hapa katika wakati muhimu kuamua juu ya utayari wa Israel mahali hapa muhimu hadi pale mpango mwingine utakapofikiwa unaohakikisha usalama wa Israel," alisema Netanyahu.

Israel ilichukua udhibiti wa eneo hilo la kusini mwa Syria kwenye mpaka na eneo la mlima Golan siku chache baada ya Rais Bashar Al-Assad kuondolewa madarakani na waasi.

Maofisa walieleza hatua hiyo ni ya muda ili kuhakikisha usalama wa mipaka ya Israel, lakini hawajatoa muda kamili wa kubaki wanajeshi hao katika eneo hilo.

Wiki iliyopita, waziri wa ulinzi Israel Katz aliagiza wanajeshi kujiandaa kubaki kwenye eneo la mlima Hermon katika msimu wa baridi.

**DW**

# Papa Francis asimulia alivyonusurika kuuawa Iraq

**VATICAN, Roma**

NJAMA za kumuua kiongozi wa kanisa la Katoliki duniani, Papa Francis, wakati alipofanya ziara nchini Iraq 2021, zilizuiliwa na majasusi wa Uingereza.

Katika kitabu cha Papa Francis, ambacho kipo katika hatua ya mwisho kuchapishwa, kiongozi huo alikiri kwamba washambualiaji wawili wa kujitoa muhanga walihusika kutaka kumuua.

Alisema kabla ya safari hiyo wasaidizi wake walimtahadharisha kuhusu njama hizo, lakini aliendelea kusisitiza ziara hiyo isiahirishwe.

Hata hivyo, washambuliaji wote wawili walikamatwa na kuuawa, alisema katika sehemu ya kitabu hicho zilizochapishwa na gazeti la Italia Corriere della Sera. Ziara hiyo, ambayo ilifanyika kwa muda wa siku tatu wakati wa janga la corona, ilikuwa ya kwanza kufanywa na papa Francis nchini Iraq.

Miaka iliyopita Iraq ilishuhudia kuongezeka kwa ghasia za kimadhehebu ya dini kati ya Waislamu wa Shia na Sunni.

Katika sehemu za wasifu wake, Papa Francis alisema karibu kila mtu alimshauri dhidi ya hatari katika ziara hiyo lakini yeye alihisi anapaswa kwenda.

Alisema njama hiyo ilifichuliwa na idara ya ujasusi ya Uingereza, ambayo walionya polisi wa Iraq, kwa upande wake alielezwa maelezo ya usalama mara tu alipowasili.

"Mwanamke aliyejaa vilipuzi, kijana mlipuaji wa kujitoa mhanga, alikuwa akielekea Mosul kujilipua wakati wa ziara ya papa," alisema.

Papa aliongeza kuwa alimuuliza afisa wa usalama siku iliyofuata kuwa nini kiliwapata washambuliaji hao, alijibiwa kuwa wote waliuawa baada ya kukamatwa. Kitabu hicho kinachoitwa Hope, kinatarajiwa kuchapishwa Januari 14, mwakani.

Hata hivyo, Vatican haijatoa majibu kuhusu maelezo hayo.

**BBC**

# Tabora United FC yalia na Mwambusi

**Na Adam Fungamwango**

MAKOCHA, Anicet Makiadi wa Tabora United na Juma Mwambusi wa Coastal Union, kila mmoja amempongeza mwenzake kwa kutumia mbinu za kuzuia vyema na kupelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora juzi kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Jeremiah Ntambwe aliifungia Coastal Union bao dakika za nyongeza za kipindi cha kwanza, huku Banele Sikhondze akisawazisha dakika ya 56 ya mchezo.

Mwambusi alisema pamoja na uchovu wa safari, walitawala mechi hiyo kipindi cha kwanza na nia yao ilikuwa ni kuimaliza mechi kipindi cha pili lakini tatizo kubwa ilikuwa ni kocha mwenzake, Makiadi kushtukia mtego na kuutegua.

"Niwapongeze wachezaji wangu kwa sare hii kwa sababu walikuwa na uchovu wa safari, lakini walijitahidi kupambana na timu ngumu ya Tabora United ikiwa nyumbani kwao. Tuliukamata mchezo kipindi cha kwanza, lakini wachezaji wangu hawakutumia nafasi licha ya niliwaambia tumalize mchezo mapema. Tunawapongeza wapinzani wetu na kocha wao kwa sababu wametuzuia kwenye mbinu zetu tulizoziweka," alisema Mwambusi.

Naye Makiadi, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alisema pamoja na kucheza nyumbani kwao, mchezo huo haukuwa rahisi kwa sababu walisumbuliwa na wapinzani wao kipindi cha kwanza.

Makiadi alisema hata kipindi cha pili walipoamka na kutawala mechi, wapinzani wao walishtukia mbinu hiyo na kubadilisha mfumo, kitu ambacho kiliwasaidia Coastal kupata sare.

"Haikuwa rahisi, mwanzo wa mchezo Coastal walitusumbua sana wakapata bao la kwanza, ila nawapongeza wachezaji wangu kwa kupambana na kuweza kusawazisha kipindi cha pili. Tungeweza kabisa kushinda, lakini kocha wao alishtukia mtego na kubadili mfumo, nampongeza sana kwa hilo, vinginevyo tungeibuka na ushindi," alisema Mwambusi.

Sare hiyo imeifanya Tabora United kufikisha pointi 25 huku Costal Union imefikisha pointi 17 na kusogea nafasi ya 10 ya msimamo wa ligi hiyo, timu zote hizo zikiwa zimemaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza.

# BAO LA DIAO LAMFURAHISHA TAOUSSI, AWAZA TIKETI CAF

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, amesema mbali na furaha ya timu yake kupata ushindi, aanika amefurahi zaidi kwa straika wake, Allasane Diao, kufunga bao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Fountain Gate iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi jioni.

Katika mchezo huo, Azam ilipata ushindi wa mabao 2-0, Diao akifunga bao la pili muda mfupi kabla ya mchezo kumalizika, huku goli la kwanza likiwekwa kimiani na winga machachari, Gilbril Sillah.

Kocha huyo alisema alimwandaa nyota huyo kuingia kipindi cha pili na alimtabiria atafunga bao.

Alisema aliamua kumwingiza mchezaji huyo ambaye hajaonekana uwanjani kwa siku nyingi kutokana na majeraha, ili aanze kuzoea mikiki mikiki ya ligi.

„Nina furaha sana kwa sababu nimeshinda, nimepata pointi tatu, tumeendelea kukwea juu kuelekea katika mbio za ubingwa au kucheza mechi za kimataifa msimu ujao, lakini nilichofurahi zaidi ni Diao kufunga bao, nilimwambia nitakupanga katika mchezo huu, utaingia kipindi cha pili na utafunga bao, kweli ikawa hivyo, hata alivyopachika bao mliona alikuja kwangu kushangilia," alisema Taoussi.

Straika huyo raia wa Senegal, alisajiliwa na Azam FC mwaka jana, akitokea klabu ya US Goree ya nchini kwao, na kabla ya kuumia amekuwa akilaumiwa kwa kushindwa kufanya kile ambacho timu na mashabiki wa timu hiyo walikitarajia kutoka kwake.

Taoussi raia wa Morocco, alisema ushindi huo haukupatikana kirahisi bali ulitokana na wachezaji wake kupambana na kuongeza kwa sasa wameshamwelewa na kufahamu mifumo yake ya uchezaji. Naye Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Mohamed Muya, alisema kilichoamua matokeo katika mchezo huo ni ubora na viwango vya wachezaji wa Azam na si vinginevyo.

"Nilijiandaa kwenda kuchukua pointi tatu dhidi ya timu ngumu, niliwapa wachezaji wangu kila mbinu ambayo tulitakiwa kuitumia katika mchezo huu na tulitengeneza nafasi, bahati mbaya hatukuzitumia nafasi zote. Ila yote kwa yote, niwapongeze wachezaji wangu wamejitahidi, ukiangalia gharama ya kikosi chetu na cha wenzetu ni tofauti, wakati mwingine viwango vya wachezaji vinaamua mechi, tunapambana katika mechi nyingine zinazofuata," alisema Muya.

Ushindi huo umeifanya Azam kuendelea kung'ang'ania kileleni katika msimamo ikifikisha pointi 33, lakini tayari ikiwa imemaliza michezo yake 15 ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu huku Fountain Gate ikisalia na pointi 20, ikiwa imecheza michezo 14 na kwenye msimamo iko nafasi ya sita.




Kipa wa JKT Queens, Najiath Abbas (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa Yanga Princess, Arieth Udong, katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. JKT Queens ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# JKT Queens kileleni TWPL

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Yanga Princess, straika wa JKT Queens, Fatuma Makusanya, amesema siri ya mafanikio ya kikosi chao ni kufuata vyema maelekezo ya benchi la ufundi.

JKT Queens sasa imefikisha pointi 17 ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba Queens yenye pointi 16, lakini imecheza mechi moja pungufu.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex juzi, Makusanya alisema utulivu na kufuata maelekezo wanayopewa mazoezini ndio yamewasaidia kupata ushindi.

"Kikubwa ni kufanya kile ambacho tunakifanya mazoezini, nilipoingia uwanjani nilikuwa nawaza kufanya kile nilichoelekezwa na kocha, na ndio kimesaidia kufunga bao," alisema Makusanya.

Aliongeza licha ya ushindi waliopata, bado amekiri ligi ya msimu huu ni ngumu na ina ushindani.

"Nitasema msimu ni mzuri pale ligi itakapomalizika, siwezi kusema kwa sasa kwa sababu bado hatujamaliza msimu, ila ligi ni ngumu na ina ushindani katika kila mechi," nyota huyo wa zamani wa Twiga Stars alisema.

Ligi hiyo itaendelea tena keshokutwa kwa Mashujaa Queens kuwakaribisha Simba Queens kwenye Uwanja wa Isamuhyo.

## ZISIKUPITE

### AGARNACHO KUTUA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid inafikiria kumnunua winga wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Argentina, Alejandro Garnacho, katika dirisha dogo la usajili la Januari, ***(Fichajes)***

### DIALLO MAMBO SAFI

MANCHESTER United ipo katika mazungumzo ya hali ya juu ili kuongeza mkataba wa winga wa Ivory Coast, Amad Diallo, mwenye umri wa miaka 22, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika msimu ujao. ***(ESPN)***

### DYBALA KUONDOKA ROMA

KOCHA wa AS Roma, Claudio Ranieri amesema fowadi wa Argentina, Paulo Dybala, mwenye umri wa miaka 31 anaweza kuondoka katika klabu hiyo ikiwa hana furaha, baada ya wakala wake kukutana na Galatasaray. ***(Corriere dello Sport)***

### MUANI ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inaweza kupambana na RB Leipzig inayoshiriki Ligi Kuu Ujerumani (Bundesliga), kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufaransa, Randal Kolo Muani, mwenye umri wa miaka 26 kwa mkopo mwezi Januari. ***(Football Insider)***

### TZIMAS AGOMBEWA ULAYA

CHELSEA, Aston Villa, Stuttgart na Newcastle United zinavutiwa na mshambuliaji wa kimataifa wa PAOK na Ugiriki, Stefanos Tzimas, mwenye umri wa miaka 18 ambaye amecheza kwa mkopo Nurnberg. ***(ESPN)***

### ROHL, SHEFFIELD KUTETA

MAZUNGUMZO bado yanaendelea kati ya Southampton na Kocha wa Sheffield Wednesday, Danny Rohl, kuhusu nafasi ya ukocha katika klabu ya St. Mary's. ***(Sky Germany)***

### ATUBOLU ANUKIA WEST HAM

KLABU ya West Ham imekuwa ikimsaka golikipa wa Freiburg mwenye umri wa miaka 22, Noah Atubolu. ***(Fabrizio Romano)***

### BURNEL YAMTAKA SONNE

KLABU ya Burnley ipo kwenye mazungumzo ya juu zaidi ya kumsajili beki wa kulia wa Peru, Oliver Sonne, mwenye umri wa miaka 24 kutoka Silkeborg kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 2.5. ***(Football Insider)***

### ROWETT KUTUA OXFORD

KOCHA wa zamani wa Birmingham City na Millwall, Gary Rowett yuko kwenye mazungumzo ya kina na Oxford United kuhusu nafasi yao ya ukocha. ***(John Percy/ Telegraph)***

### ARAUJO, DE JONG WAONYWA

BARCELONA imewaonya, Ronald Araujo, mwenye umri wa miaka 25, na kiungo wa kati, Frenkie de Jong (27), kuhusu kusaini mikataba mipya katika klabu hiyo la sivyo wakabiliwe na uwezekano wa kutakiwa kuhama. ***(Sport)***

### IGAMANE ANUKIA EVERTON

EVERTON inamfuatilia mshambuliaji wa Rangers na Morocco, Hamzane Igamane, mwenye umri wa miaka 22, huku mustakabali wa mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin (27), na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Beto (26), katika klabu hiyo haueleweki. ***(TBR Football)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS JR MCHEZAJI BORA WA FIFA 2024

●●● Mbrazil huyo amekuwa na msimu mzuri huku mabao yake...

**PARIS, Ufaransa**

VINICIUS Junior ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora wa mwaka wa FIFA 2024 baada ya kuwa na msimu wenye mafanikio bora akiwa na Real Madrid.

Mbrazil huyo alikosa tuzo ya Ballon d'Or Oktoba, mwaka huu, lakini hajapuuzwa katika usiku wa kuamkia jana katika tuzo hizo za FIFA, ambao wamemtaja mchezaji bora zaidi kufuatia uchezaji wake wa kuvutia kwa klabu na nchi.

Vinicius alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na taji la Ligi Kuu Hispania (LaLiga), katika kipindi cha msimu uliopita na kufunga jumla ya mabao 24 katika mashindano yote.

Msimu huu pia ameanza pale alipoishia, akiongeza mabao 13 zaidi kwa Real Madrid kufikia sasa.

Kilele cha mwaka mzuri kilikuwa katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa Juni, Vinicius alifunga bao la pili wakati wa ushindi wa 2-0 dhidi ya Borussia Dortmund huku Los Blancos wakitwaa taji lao la 15.


Hii ni mara ya kwanza kwa Vinicius kushinda tuzo hiyo, iliyoanza kutolewa mwaka 2016, na ndiye Mbrazil pekee aliyeshinda tuzo hiyo hadi sasa. Hapo awali Neymar alikaribia zaidi, lakini alimaliza nafasi ya tatu mwaka 2017.

Cristiano Ronaldo na Luka Modric ndio wachezaji wengine pekee wa Real Madrid walionyakua tuzo hiyo ya FIFA, huku Lionel Messi ndiye mshindi wa hivi karibuni zaidi mwaka 2023.

Katika tuzo za Ballon d'Or ya 2024 Vinicius alishindwa na nyota wa Manchester City, Rodri.

Real Madrid ilitoa wachezaji watano waliowania tuzo hiyo, akiwamo, Toni Kroos ambaye sasa amestaafu, huku Jude Bellingham, Kylian Mbappe, Dani Carvajal na Federico Valverde pia wakiwa kwenye orodha hiyo.

# Foden: Mambo magumu City



**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Phil Foden, alifichua ndani ya chumba cha kubadilishia nguo cha mabingwa hao wa Ligi Kuu England kilikuwa "cha huzuni sana" baada ya kufungwa na Manchester United Jumapili iliyopita.

Foden alirejea katika kikosi cha kwanza cha City baada ya kupona jeraha, lakini alijitahidi kufanya mashambulizi kwenye pambano ambalo lilikuwa limekwama.

Vijana wa Pep Guardiola licha ya kuanza kufunga bao kupitia kwa Josko Gvardiol akiunganisha na krosi ya Kevin De Bruyne, lakini wakaangukia pua.

Akitafakari mara baada ya mechi hiyo, Foden alisema: "Siwezi kuweka kidole kwenye kile kinachoendelea. Nilidhani uchezaji ulikuwa mzuri zaidi ya kupata matokeo, lakini tulitoka bila pointi, na inaonekana haikuwa sawa kabisa.

"Chumba cha kubadilishia nguo ni dhahiri kitakuwa chini na cha kusikitisha," aliongeza Foden.

"Ni juu ya kuweka mawazo yetu kuwa na nguvu kwa muda wote wa dakika 90 na hatufanyi hivyo kwa sasa. Inabidi twende tena na kuonesha tabia ili kurejea kutoka kwenye sura hii. Sio wakati wa kulalamika - ni juu ya kushikamana, kubaki na nguvu na kwenda tena nina uhakika tutarudi."

# FA yamsimamisha Mudryk, akanusha

**LONDON, England**




MCHEZAJI wa Chelsea ambaye ni raia wa Ukraine, Mykhailo Mudryk, mwenye umri wa miaka 23 amesimamishwa kwa muda kucheza baada ya vipimo vilivyofanywa na Chama cha Soka England (FA) kuonyesha anajihusisha na utumiaji wa dawa za kusisimua misuli zilizokatazwa michezoni.

Klabu ya Chelsea imethibitisha taarifa hizo na kusema FA imeshawasiliana na mchezaji huyo kuhusu 'majibu yasiyofaa' katika vipimo vya mkojo vilivyofanyika hivi karibuni vilivyohusisha wachezaji wote wa klabu hiyo.

Mudryk ameithibitishia klabu yake hajawahi kutumia dawa hizo za kusisimua misuli akiwa anajua au kutumia kitu chochote kile kilichopigwa marufuku katika mchezo wa mpira wa miguu.

Mchezaji huyo pamoja na klabu yake kwa pamoja wanashughulikia kujua sababu za kupatikana kwa majibu yaliyoonyesha mchezaji huyo anatumia dawa zilizopigwa marufuku.

Paul Pogba, mchezaji wa zamani wa Juventus na Manchester United, alifungiwa kwa miaka mitatu kujihusishwa na soka kwa kosa kama hilo, lakini adhabu yake ilipunguzwa hadi kubakia miezi 18.



# RASHFORD: NIKO TAYARI KUONDOKA MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

MARCUS Rashford amedokeza kuhusu kuondoka Manchester United kwa kusema "niko tayari kwa changamoto mpya" baada ya kukiri "nilikatishwa tamaa" baada ya kuondolewa katika kikosi cha Kocha, Ruben Amorim, kilichoshinda dabi dhidi ya Manchester City.

Rashford mwenye umri wa miaka 27 na winga, Alejandro Garnacho, hawakujumuishwa katika kikosi kilichoshinda mabao 2-1 mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Etihad Jumapili iliyopita.

Amorim alieleza uamuzi wake kwa kusema "uchezaji katika mazoezi, utendaji katika mchezo, jinsi unavyovaa, jinsi unavyokula, jinsi unavyoshirikiana na wachezaji wenzako" yote yalikuwa mambo muhimu.

Kiwango cha Rashford msimu huu kimemfanya fowadi huyo kupoteza nafasi yake ya kuanzia katika kikosi cha kwanza.

Pia amekuwa na masuala ya nje ya uwanja katika miezi ya hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na kuachwa na makocha wa zamani Erik ten Hag kwa kukosa mikutano ya timu na vipindi vya mazoezi.

Pia aliondolewa katika safari ya mechi ya Kombe la FA mjini Newport msimu uliopita baada ya mapumziko ya usiku mjini Belfast.

Amorim, ambaye alichukua nafasi ya Ten Hag kama kocha mwezi uliopita, aliweka wazi wachezaji wote wawili wataanza wiki hii wakiwa na mchezo safi.

Hata hivyo, Rashford sasa amezungumza kwa mara ya kwanza tangu kuondolewa dhidi ya City na ametoa dalili wazi yuko tayari kuondoka Old Trafford, karibu miaka tisa baada ya kucheza mechi yake ya kwanza akiwa na umri wa miaka 18.

"Kwangu mimi binafsi, nadhani niko tayari kwa changamoto mpya na hatua zinazofuata," alisema Rashford akimwambia mwandishi, Henry Winter wakati wa hafla katika shule moja huko Manchester.

"Ninapoondoka itakuwa 'hakuna hisia ngumu.' Hutakuwa na maoni yoyote mabaya kutoka kwangu kuhusu Manchester United. Huyo ni mimi kama mtu.

"Ikiwa najua kuwa hali tayari ni mbaya, sitafanya kuwa mbaya zaidi. Nimeona jinsi wachezaji wengine walivyoondoka siku za nyuma na sitaki kuwa mtu huyo.

"Nikiondoka nitatoa taarifa na itakuwa kutoka kwangu, inakatisha tamaa kuachwa kwenye dabi, lakini imetokea, tukashinda mchezo kwa hiyo tuendelee.

"Inasikitisha, lakini pia mimi ni mtu kwa vile nimekuwa mkubwa naweza kukabiliana na vikwazo."

Rashford alitia saini mkataba wa nyongeza uliomfanya alipwe pauni 325,000 kwa wiki wa miaka minne na nusu pale United Julai, mwaka jana na angeamuru ada kubwa ya uhamisho ikiwa klabu itasikiliza ofa za mchezaji huyo katika dirisha la uhamisho la Januari.

Vyanzo vimeiambia ESPN nia iliyotoka kwa klabu yoyote ya Ulaya kwa Rashford na mahali panapowezekana zaidi katika siku zijazo itakuwa Ligi ya Saudi Arabia.

Rashford mzaliwa wa Manchester amekuwa akikosolewa na mashabiki wa klabu hiyo.

"Ninahisi kutoeleweka, lakini siko sawa," alisema.

"Mimi ni mtu rahisi sana. Ninapenda soka. Hayo yamekuwa maisha yangu tangu mwanzo.

HABARI MICHEZO

# SIMBA, YANGA, TP MAZEMBE 'KUIBOMOA' FOUNTAIN GATE

**Na Adam Fungamwango**

KLABU za Simba, Yanga na TP Mazembe zimetajwa kupeleka ofa katika klabu ya Fountain Gate kwa ajili ya kuhitaji nyota wa timu hiyo katika dirisha dogo la usajili lililofunguliwa hivi karibuni, imefahamika.

Habari kutoka Fointain Gate zinasema Simba imepiga hodi ikitaka huduma ya straika, Edgar William wakati Yanga wanamhitaji beki wa kushoto, Laurian Makame na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, imeweka nia ya kumsajili, Selemani Mwalimu.

Chanzo hicho kimesema klabu hizo zimewasilisha ofa zao na tayari zimeanza kufanyiwa kazi.

"Hapa kuna ofa tatu, sasa kama tutazikubali zote ili na sisi tufanye usajili kipindi hiki, au tutoe mchezaji mmoja wengine tuwaache au wawili. Na pia tunataka kuangalia ni sehemu gani ambazo tukitoa wachezaji hatutoathirika zaidi, ni vitu vingine tu tutaangalia kabla ya kufanya uamuzi,“ kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza TP Mazembe inamhitaji Mwalimu ambaye tayari ameshafunga mabao matano mpaka sasa katika Ligi Kuu Tanzania Bara, akishika nafasi ya pili nyuma ya Elvis Rupia wa Singida Black Stars mwenye mabao saba.

"Mazembe wamebaini wanahitaji kujiimarisha, wameona wanaudhaifu kwenye eneo la ushambuliaji ambalo linawagharimu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hatua ya makundi,“ kiliongeza chanzo hicho.

Edgar, ambaye pia ana mabao matano anahitajiwa na Simba ili kwenda kutoa ushindani kwa mastraika wengine akiwamo, Steven Mukwala na Leonel Ateba, huku Makame akitakiwa na Yanga ili kwenda kuimarisha eneo la beki wa pembeni.

Akizungumzia hilo, Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Mohamed Muya, alisema binafsi hajapata taarifa yoyote kutoka kwa viongozi kama wamepokea ofa ya kutakiwa wachezaji hao.

Muya alisema hana hofu yoyote kama wachezaji hao wataondoka, na badala yake watatengeneza nyota wapya na hiyo ndiyo ‚biashara‘ ya soka inavyokwenda.

"Kazi yetu walimu ni kutengeneza wachezaji, ukiangalia tulisalia na wachezaji sita tu wakati tunaitwa Singida Big Stars, baada ya wengi kupelekewa Ihefu FC ambayo ilibadilishwa ikawa Singida Black Stars, lakini tulipata wengine tukawatengeneza na watu wameanza kuwatolea macho.

Hata sisi tunawaombea vijana tunaowatengeneza wasonge mbele, waende mbali wapate mafanikio, sijapata taarifa rasmi kutoka kwa viongozi, lakini kama ni hivyo tunawaombea baraka, Mungu awajalie wanakokwenda, tutapata wengine nao watakuwa kama hawa,“ alisema kocha huyo.



Kiungo wa Serengeti Boys, Razak Mbegelengi (kushoto), akijipanga kumdhibiti mchezaji wa Kenya katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-17), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nakivubo jijini, Kampala Uganda jana. Serengeti Boys ilishinda bao 1-0. **PICHA: TFF**

# Serengeti Boys yatinga nusu fainali

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), imetinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-17), baada ya kuifunga Kenya bao 1-0 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nakivubo jijini, Kampala nchini Uganda jana.

Ushindi huo unaifanya Serengeti Boys kufikisha pointi nne na kuwa kinara katika Kundi A.

Mechi nyingine ya Kundi A itawakutanisha wenyeji Uganda na Kenya.

Serengeti Boys inashiriki mashindano hayo kwa ajili ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-17).

Katika mechi ya kwanza ya Kundi A, Serengeti Boys ilitoka sare ya bao 1-1 na wenyeji Uganda.

Sudan Kusini watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-0 waliopata katika mechi ya kwanza ya Kundi B dhidi ya Somalia.

Fainali ya mashindano hayo yanayoshirikisha timu sita kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), itachezwa Desemba 27, mwaka huu.

## Polisi Tanzania FC kutoa zawadi Jpili

**Na Restuta James**

TIMU ya Polisi Tanzania, imeahidi kupata ushindi mnono ambao utakuwa zawadi ya sikukuu za mwisho wa mwaka kwa mashabiki wa klabu hiyo kwa kuifunga Songea United katika mechi ya Ligi ya Championship itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika Moshi mkoani, Kilimanjaro.

Ofisa Habari wa Polisi Tanzania FC, Inspekta, Frank Lukwaro, alisema kikosi chao kipo imara na kinaendelea vyema na maandalizi ili kuhakikisha wanapata alama tatu muhimu katika mchezo huo wa nyumbani.

"Mkoa wa Kilimanjaro una utamaduni wa kupokea wageni na wenyeji wengi kila mwisho wa mwaka, hivyo tunawaomba waje kwa wingi ili waweze kupokea zawadi ya ushindi kwa sababu tunajua shabiki ni mchezaji wa 12 uwanjani na tumejipanga kufanya vizuri katika mchezo huu," alisema Lukwaro.

Alisema benchi la ufundi pamoja na wachezaji wote wameweka mikakati ya kuondoka na alama hizo tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Kwa sasa Polisi Tanzania iko katika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 13 kibindoni baada ya kucheza michezo 12.

## Azam FC yawaalika KVZ kuwapa nguvu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIKA kuhakikisha kikosi chake kinaendelea kujiweka imara, Azam FC inatarajia kukutana na KVZ kutoka Zanzibar katika mechi ya kirafiki itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Tayari kikosi cha KVZ kimeshawasili jijini kwa ajili ya mchezo huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa KVZ, Abduljalili Mohamed, alisema lengo la kucheza mchezo huo wa kirafiki ni kujiandaa na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar pamoja na mashindano ya Kombe la FA.

Mohamed alisema katika kuelekea mzunguko wa pili benchi la ufundi la timu yao lilihitaji kucheza michezo mingi ya kirafiki na timu za ligi tofauti ili kuwaongezea uzoefu wachezaji wao.

"Tumeanza na Azam FC kwa sababu tunajua ni miongoni mwa timu ambazo zinafanya viuzri katika Ligi Kuu Tanzania Bara, kuwapo na wachezaji wazuri wa ndani na nje ya Tanzania itatusaidia kutupa mwanga, tutakuwa pia tayari kuanza vyema mzunguko wa lala salama,“ alisema ofisa huyo.

KVZ FC ni moja ya timu zilizoko katika mbio za kusaka ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Vinicius Jr Mchezaji Bora wa FIFA 2024 UKURASA 21

# Michezo


Alhamisi Desemba 19, 2024
Nipashe



# SIMBA YAENDELEZA DOZI LIGI KUU BARA

## Straika wake Ateba moto chini, afikisha mabao matano...

**Na Adam Fungamwango**



Mshambuliaji wa Simba, Leonel Ateba (jezi nyekundu), akifunga bao la pili huku amekabwa na wachezaji wa KenGold FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

MABAO mawili yaliyofungwa na straika Mcameroon, Leonel Ateba, yaliiwezesha Simba kuondoka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KenGold katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana.

Matokeo hayo yanaifanya Simba kukaa katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kutimiza pointi 31.

Mabao hayo ya jana pia yanamfanya straika huyo kufikisha magoli matano katika ligi hiyo, ikiwa ni mara yake ya kwanza kucheza nchini baada ya kusajiliwa mwanzoni mwa msimu huu, akitokea USM Alger ya Algeria.

Ateba alifunga bao la kwanza dakika ya 35 kwa penalti, iliyotolewa na mwamuzi, Esther Adalbert, kutoka mkoani, Singida baada ya beki wa kushoto, Bilal Amin, kumkwatua, Awesu Awesu, ndani ya eneo la hatari.

Dakika moja kabla ya kwenda mapumziko, straika huyo alifunga bao la pili kwa kichwa baada ya kuunganisha vyema mpira wa kona iliyopigwa na Valentino Nouma na kuwanyanyua tena mashabiki wa Simba ambao Jumapili iliyopita walipata ushindi mwingine katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ateba aliruka juu kuliko wachezaji wote na kuukwamishwa wavuni, likiwa ni bao la pili na la mwisho katika mchezo huo.

Ushindi wa jana ni wa 10 kwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadlu Davids, tangu apewe majukumu ya kukiongoza kikosi hicho kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Simba ilianza mchezo kwa kulishambulia mfululizo lango la KenGold, wakisaidiwa na mfumo wa wapinzani wao wa kukaa nyuma ya mpira na kuacha wao kutawala, huku wakiziba mianya.

Sekunde ya 39 tu, Kibu Denis akiwa kiasi cha mita takriban 30 hivi alipiga shuti lililotoka nje kidogo la lango, akiwa amepata pasi kutoka kwa Ateba.

Ni kama alikuwa amepata maelekezo kutoka Fadlu, kwa sababu alifanya tena majaribio hayo dakika ya pili na tano ya kupiga mashuti ya mbali kutokana na KenGold kurundikana langoni, lakini la kwanza lilipaa juu kidogo ya lango na jingine lilidakwa na kipa, Castor Mhagama.

Nouma, naye alimuiga Kibu, alipojaribu shuti la mbali dakika ya sita, lakini Mhagama alikuwa macho na kulidaka kwa ustadi mkubwa.

Baada ya kushindwa kupata mabao ya mapema, wachezaji wa Simba walionekana kupunguza kasi na kuanza kupigiana pasi fupi fupi huku wakijaribu kuifungua safu ya ulinzi ya wageni wao bila mafanikio.

Hatimaye, KenGold ilifanya shambulio la kwanza katika lango la Simba, dakika ya 26, Helbert Lukindo alipopata nafasi ya kubaki na kipa, Moussa Camara kutokana na makosa ya mabeki, lakini kipa huyo raia wa Guinea alikuwa makini na kuunyaka mikononi mpira huo.

'Tik-tak' ya Chamou Karaboue, nusura iipatia Simba bao dakika ya 30, akiunganisha krosi ya Ateba, lakini Mhagama alifanya kazi ya ziada, akaudaka mpira huku Abdallah Masoud 'Cabaye', alikaribia kuifungia KenGold bao sekunde chache kabla ya mapumziko, lakini Camara alikaa imara na kudaka shuti hilo.

Kipindi cha pili kilikuwa ni cha KenGold kwa sababu waliamua kufunguka na kuwapa wakati mgumu Simba.

Ateba angeweza kupata 'hat-trick' ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kama shuti lake la mguu wa kushoto, akiunganisha krosi ya Ahoua, lisingetoka sentimeta chache, langoni mwa KenGold sekunde chache kabla ya mechi kumalizika, likiwa ndiyo shambulizi kubwa kwa timu hiyo kipindi chote cha pili.

KenGold imemaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza, ikiwa na pointi sita tu, ikiendelea kuburuza mkia kwenye ligi.

## Yanga, Mashujaa mechi ya ufundi

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kutoka katika mashindano ya kimataifa, mabingwa watetezi, Yanga wanatarajia kuwakaribisha Mashujaa FC kutoka Kigoma katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam huku makocha wakitamba utakuwa mchezo wa ufundi zaidi.

Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema ameiangalia vizuri Mashujaa na kubaini ni timu nzuri, hivyo inakwenda kuwakabili kwa tahadhari na watatumia mifumo tofauti katika mechi hiyo.

Ramovic alisema anaweza kubadilisha mfumo kutokana na mchezo utakavyokuwa unaendelea kwa lengo la kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

"Najua tunatakiwa tuonyeshe sisi ni nani, kila timu tunaiheshimu na kila mechi tunakwenda kucheza kwa plani tofauti, tunahitaji kushinda na kukaa sehemu salama, kwa sababu mechi zimekuwa nyingi sasa za ligi kuu na timu zilizo juu zimekuwa zikipata ushindi.

Kama hatuweka mkazo, kupambana kwenye mchezo huwezi kushinda, kama huwezi kukimbia uwanjani kama una mpira na kumkimbiza mpinzani wakati hauna mpira, basi huwezi kufanya kitu, tumemuangalia mpinzani wetu na tunajua jinsi gani tunakwenda kupamba naye kimbinu na kifundi," alisema Ramovic.

Kocha huyo pia amewaomba wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa wavumilivu kwa sababu bado ana muda mchache sana tangu alipojiunga na katika kikosi hicho.

"Kama nilivyosema nimekuja hapa nina wiki tatu tu, sina 'pre season',nimekuta timu imepoteza wachezaji muhimu wanne kwa majeraha, haiwezi kuwa rahisi, lakini hakuna hata mmoja anayetaka kujua kuhusu hilo,wanachohitaji ni matokeo moja kwa moja, ukweli ni presha kubwa lakini kwangu ndicho kitu ambacho nimezoea kuishi, tupo hapa kufanya kazi ili tushinde mechi za Ligi Kuu, kuhusu Ligi ya Mabingwa si muda wake hivi sasa," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Mashujaa, Abdallah Mohamed 'Bares', alisema timu yake inazihitaji zaidi pointi tatu kwa 'udi na uvumba'.

Sina shaka utakuwa ni mchezo wa kimbinu zaidi na kiufundi, tunajua Yanga ni timu inayochezea sana mpira ina viungo wazuri, ila sisi ni timu ambayo tunabadilika kutokana na timu tunayocheza nayo kwa hiyo tunatakikisha tunawadhibiti katika maeneo hayo, mbinu nyingine si vyema sana kuisema hapa,"alisema Bares.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >